# Nipashe

Jumamosi Agosti 3, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579987
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
w.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## MO kuwekeza bil. 860/- kumwaga ajira 100,000

UKURASA 2




UKURASA 13

# Polisi yatoa msimamo usafiri mabasi saa 24

• **Yapiga** marufuku baadhi ya mikoa sababu za kiusalama, pia kutoka wilaya moja kwenda nyingine... *Endelea ukurasa wa 2*



## Lugola akingia kifua bodaboda

UKURASA 3

UKURASA 3

Wagonjwa wanne waliopandikizwa figo kwenye kambi maalum ya wiki moja katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), (kutoka kushoto), Othniel Kimaro wa Tanga, Gasper Metta wa Singida, Ramadhani Munna wa Dar na Dominic Uledi wa Mtwara, wakiwa na Muuguzi wa Chumba cha Wagonjwa Mahututi cha hospitali hiyo, Elizabeth Stephen (kulia) baada ya kuruhusiwa jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Muhimbili yaokoa bilioni 5/- upandikizaji figo wagonjwa

**MICHEZO** **YANGA WAINOGESHA SIKU YA MWANANCHI** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Aliyemrithi Lissu afunguka

**Na Elisante John,** SINGIDA

MIRAJI Mtaturu, Mbunge mteule wa Singida Mashariki (CCM), ametaja vipaumbele vinne katika mwaka mmoja wa ubunge wake jimboni huko.

Mtaturu amepitishwa kuwa mbunge wa jimbo hilo baada ya wapinzani wake 12 kushindwa kurejesha fomu kwa msimamizi wa uchaguzi.

Kiti cha ubunge wa jimbo hilo kilitangazwa kuwa wazi na Spika Job Ndugai Juni 28, mwaka huu kutokana na kile alichoeleza kuwa aliyekuwa mbunge wake, Tundu Lissu (Chadema) ni mtoro bungeni na hajajaza fomu ya mali na madeni na kuiwasilisha kwenye mamlaka husika.

Akizugumza baada ya kukabidhiwa cheti cha ushindi kwenye hafla iliyofanyika kwenye Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Mtaturu alisema kipaumbele chake cha kwanza ni elimu.

Alivitaja vipaumbele vingine katika mwaka huo mmoja wa ubunge wake kuwa ni afya, maji na mindombinu, hasa barabara.

Alisema amelazimika kuanza na elimu kutokana na kuzorota kwa sekta hiyo kwa muda mrefu jimboni mwake huku wananchi wakiwa na kiu ya kuona watoto wao wanasonga mbele kitaaluma.

"Lazima watoto wetu wapate fursa ya kusoma, nilipokuwa DC (Mkuu wa Wilaya), niliandika andiko la Sh. bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha ufundi na tayari serikali imekubali kuipatia wilaya yetu Sh. bilioni mbili ili zianze kujenga chuo hiki," alisema.

Kuhusu sekta ya afya, Mtaturu alisema ameiomba Sh. bilioni moja na tayari imeipatia wilaya hiyo Sh. milioni 500 ili kujenga hospitali ya wilaya.

Mbunge huyo mteule alisema tayari serikali imeipatia wilaya hiyo visima vinane. Kati yake, vitano tayari vimechimbwa kwenye Jimbo la Singida Mashariki.

Aliongeza kuwa serikali imeahidi kutoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kujenga miundombinu na kutandaza mabomba ya maji kwenye jimbo hilo ili kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa maji kwa wananchi.

Kuhusu miundombinu, Mtaturu aliahidi kufuatilia serikalini kuona namna ya kutatua changamoto aliyodai imekuwa kero kwenye jimbo hilo kwa kipindi kirefu.

Alisema amepata jeuri ya kusema hayo baada ya kupatiwa hati ya ushindi inayompa uhakika wa kuwahudumia wananchi wa jimbo hilo.

# Polisi yatoa msimamo usafiri mabasi saa 24

**Na Romana Mallya**

LICHA ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, kuagiza mabasi yaruhusiwe kusafirisha abiria saa 24, Jeshi la Polisi limetangaza mikoa ambayo huduma hiyo haitakuwapo hadi watakapojiridhisha na hali ya usalama.

Julai 7, mwaka huu, Lugola akiwa Bunda mkoani Mara aliagiza mabasi yaruhusiwe kusafirisha abiria kwa saa 24 nchini, akisitiza: "Hatuwezi kupangiwa ratiba ya kusafiri na majambazi, serikali ipo imara pamoja na polisi."

Hata hivyo, jana zikiwa ni siku 26 tangu Lugola kuzuia makamanda wa polisi wa mikoa kuzuia mabasi yanayofanya safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kanda ya Ziwa kusafiri usiku, jeshi la polisi lilitoa orodha ya mikoa ambayo agizo la waziri huyo linahitaji subira kutekelezwa.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo kutoka Makao Makuu ya Polisi, Liberatus Sabas, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema Jeshi la Polisi limeamua kufanya hivyo kwa sababu za kiusalama.

Sabas alitaja mabasi ambayo hayataruhusiwa kutembea usiku ni yale ya kutoka Dar-Kahama-Kigoma, Dar-Tabora-Katavi, Kahama-Geita-Kagera, Kahama kwenda mikoa mingine iliyopo mipakani na Dar-Tabora kwenda wilaya zake. Alisema wameamua kufanya hivyo kwa sababu maeneo hayo yana changamoto mbalimbali ambazo licha ya kwamba sasa hakuna matukio, wameamua kujipanga ili siku za usoni kusitokee madhara.

Alisema maeneo ambayo mabasi yanaruhusiwa kutembea usiku ni yale ya kutoka Morogoro-Dar na Shinyanga-Mwanza.

"Kuna sehemu ambapo mabasi yalikuwa yakifika usiku mfano Morogoro, Shinyanga na Kahama. Mabasi kutoka Dar es Salaam kuelekea Mwanza yalikuwa yanalala Shinyanga, yanayotoka Kanda ya Ziwa yanalala Morogoro.

"Tuliruhusu yatembee kwa sababu tumejipanga vizuri lakini baada ya kutafakari, tumebaini kuna maeneo mengine ambayo zoezi hilo linatakiwa kusubiri kidogo wakati tukijipanga vizuri kwa sababu za kiusalama," alisema.

Sabas alisema mabasi yanayotoka Dar es Salaam kwenda Katavi na Kigoma kupitia Tabora kwa sasa yanatakiwa yalale Tabora kwa sababu za kiusalama.

"Mabasi yaliyokuwa yakitoka Dar es Salaam kupitia Kahama kwenda Kagera nayo yalale Kahama na asubuhi yaendelee na safari. Yapo yaliyokuwa yakipita Tabora usiku sana yanakwenda kwenye wilaya zake tunataka yalale Tabora," alisema.

Aliongeza kuwa watakapojiridhisha hali ya usalama nchi nzima, mabasi yote yataruhusiwa kusafirisha saa 24 lakini kwa sasa maeneo yaliyotajwa yanatakiwa kwenda na agizo hilo.

"Muda gani wa kujiridhisha tutachukua, itategemea mpaka hali ya usalama tutakapojiridhisha, kujiridhisha ni mchakato, tunataka wasafiri salama, hata kama itakuwa wiki au miezi, tukishajipanga vizuri, wataanza," alisema.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limesema takwimu zinaonyesha makosa ya jinai makubwa na madogo yamepungua kwa asilimia moja katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka jana.

Kwa upande wa nyara za serikali, Sabas alisema katika kipindi hicho cha mwaka huu, wamekamata nyara mbalimbali za wanyama 899 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.1 zikijumuisha watuhumiwa 267.

"Zilikamatwa ngozi za chui mbili, ngozi za simba mbili, vipande vya meno ya tembo 551, twiga wawili na nyati mmoja," alisema.



Rais John Pombe Magufuli akizungumza na Mkurugenzi wa Kiwanda cha 21st Century Food and Packaging, Mohamed Dewji, baada ya kuzindua kiwanda hicho, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IKULU**

# MO kuwekeza bil. 860/- kumwaga ajira 100,000

**Na Mwandishi Wetu**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mohamed Dewji 'MO', amemweleza Rais John Magufuli kuwa kampuni zake zinatarajia kuwekeza jumla ya Sh. bilioni 860 na kutoa ajira kwa watu 100,000 katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 520 zitawekezwa kwenye viwanda na Sh. bilioni 340 zitaelekezwa katika kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari kwa lengo la kuhama kutoka kwenye biashara ya kuagiza sukari na kuwa wazalishaji wa sukari kuitikia wito wa serikali kutatua changamoto ya tatizo la sukari nchini.

MO, mmoja wa mabilionea vijana barani Afrika, aliyasema hayo wakati akimkaribisha Rais Magufuli kwenye hafla ya uzinduzi wa Kiwanda cha 21st Century Food and Packaging Limited jijini Dar es Salaam juzi.

Hafla hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo mawaziri, wakuu wa mikoa, wabunge, mabalozi, viongozi wa taasisi mbalimbali za serikali na viongozi wa dini.

Katika hafla hiyo, MO ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mohamed Interprises, alisema kiwanda ni miongoni mwa viwanda takribani 40 vinavyomilikiwa na MeTL Group wanaojishughulisha na nyanja mbalimbali za kiuchumi ikiwamo biashara za ndani na nje ya nchi.

"Kwa sasa Kampuni za MeTL Group zinatoa ajira kwa Watanzania takribani 30,000 ambao wako mijini na vijijini. Na ndiyo kampuni kubwa zaidi hapa Afrika Mashariki na Kati ikiongoza kutoa ajira kwa watu wengi zaidi," alisema.

Alisema kiwanda kilichozinduliwa juzi ni miongoni mwa viwanda vikubwa na vya kisasa kinachojihusisha na uzalishaji wa unga wa ngano na unga wa mahindi, sasa kikiwa kimewekeza kwenye mitambo mikubwa iliyogharimu jumla ya Sh. bilioni 105.

MO alimwahidi Rais Magufuli kuwa uongozi wa Kampuni ya MeTL Group utaendelea kumuunga mkono kwenye jitihada zake za kuifanya Tanzania iwe nchi ya viwanda na yenye uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.

Mfanyabiashara huyo mkubwa alibainisha kuwa wamepanga kuwekeza Sh. bilioni 520 katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwenye viwanda. Alisema uwekezaji

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Bwana shamba wa Chama cha Wafanyabiashara, Wasindikaji na Wasafirishaji wa mboga, viungo, matunda na maua nchini (TAHA), Magembe Sugwa (kushoto), akifafanua jambo kwa mkulima alietembelea banda lao, Bjarne Laustsen katika maonyesho ya Nane Nane kwa Kanda ya Kaskazini yanayofanyika katika viwanja vya Taso, eneo la Njiro, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Bil. 5/- zaokolewa upandikizaji figo

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imeokoa Sh. bilioni 4.7 kwa kupandikiza figo wagonjwa 47.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wakiwaruhusu wagonjwa wanne ambao wamepandikizwa figo, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Figo, Jackline Shoo, alisema tangu matibabu yaanze kutolewa nchini, wamefanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha.

Alisema tangu huduma ya kupandikiza figo ilipoanza mwaka 2017, hadi sasa wamewapandikiza wagonjwa 47 huku akibainisha kuwa gharama za matibabu hayo ughaibuni kwa mgonjwa ni kati ya Sh. milioni 80 na 100.

Dk. Shoo alisema huduma hiyo nchini kwa sasa inatolewa kwa gharama ya kati ya Sh. milioni 25 na 32, lakini akaeleza kuwa wagonjwa wengi wamekuwa wakitibiwa kwa gharama za hospitali kutokana na kutokuwa na uwezo wa kumudu matibabu hayo ya kibingwa.

Alibainisha kuwa kwa sasa wana wagonjwa 340 ambao wanasafisha figo na baadhi yao wanatumia mfuko wa bima na asilimia 40 wanapatiwa huduma hiyo wakiwa ni wagonjwa wa msamaha.

Alisema ugonjwa wa figo ni tatizo kubwa nchini kwa kuwa kwa mwezi hupokea wagonjwa wapya 20 ambao wanakuwa katika hatua mbaya, yaani wanahitaji kusafisha damu. "Sisi tuko zaidi katika kutoa huduma mgonjwa anapofika na kuhitaji huduma tunampatia, hatujali kama ana fedha au hana, pia kila mwezi tunapokea wagonjwa wapya wasiopungua 20.

"Wagonjwa wengi wanafika wakiwa katika hali ambayo wanahitaji huduma maalum ya kusafisha damu ama upandikizaji wa figo, hii inaonyesha kwamba upo ucheleweshaji katika kugundua mapema tatizo la figo," alisema.

Dk. Shoo alisema huenda suala hilo linachangiwa na ukosefu wa elimu kuhusiana na ugonjwa huo ama changamoto ya kutokufikia huduma hizo kwa wakati.

# Lugola awakingia kifua bodaboda

**Na Felix Mwagara,** MOSHI

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewapiga marufuku askari polisi kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani kuwalipisha faini waendesha bajaj na bodaboda papo kwa papo wanapofanya makosa barabarani na kutaka wapewe siku saba kama ilivyokuwa kwa magari.

Amesema Bajaj na Bodaboda navyo ni vyombo vya moto, hivyo madereva wakifanya makosa wanapaswa kupewa hukumu sawa na ilivyo kwa magari.

Akizungumza na mamia ya wamiliki na waendesha bajaj na bodadoda Mkoa wa Kilimanjaro katika mkutano uliofanyika Ukumbi wa CCM mjini Moshi jana, Lugola alisema bodaboda na bajaj zinatambuliwa kupitia halmashauri ya eneo husika.

Alisema vyombo hivyo vya moto vinasajiliwa, wamiliki wake wanajulikana na madereva wake wanajulikana, hivyo ukusanyaji wa faini hautakua mgumu.

"Hii haina usawa hata kidogo, eti magari yanapewa siku saba kulipishwa faini lakini bodaboda papo kwa papo, hii siyo sawa, hivyo navunja utaratibu huku nikielekeza lazima utambuzi wa vyombo hivyo ufanywe ili ulipaji wa faini usiwe na tabu yoyote," Lugola aliagiza.

Waziri huyo aliwatuliza waendesha bodaboda hao ambao sehemu kubwa walikuwa wanawalalamikia viongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kuwabadilisha vituo vya kupaki vyombo

INAENDELEA UK. 8

# CUF yaipima ubavu polisi

**Na Mary Geofrey**

HUKU kukiwa na zuio la mikutano ya kisiasa nchini, Chama cha Wananchi (CUF) kimetangaza kufanya mkutano wa hadhara leo ili kuhamasisha wananchi kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano kwa Umma wa CUF, Abdul Kambaya, ilieleza kuwa mkutano huo utakaoongozwa na Katibu Mkuu wa chama hicho, Khalifa Suleiman Khalifa, utafanyika kwenye Viwanja vya Vingunguti Relini jijini Dar es Salaam.

"Chama cha Wananchi kitafanya mkutano wa hadhara kesho (leo) katika Viwanja vya Vingunguti Relini katika kujiandaa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

"CUF imefikia uamuzi huo baada ya kauli ya Msajili wa Vyama vya Siasa Nchini, Jaji Francis Mutungi, kuwa hajapata malalamiko toka chama chochote kudai kuzuiwa na Jeshi la Polisi kufanya mikutano," Kambaya alieleza katika taarifa hiyo.

Alisema katika maandalizi ya mkutano huo, chama hicho kimemwandikia barua Mkuu wa Kituo cha Polisi Buguruni na kumpatia nakala ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

Alisema lengo ni kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye Uchaguzi wa Mitaa na

INAENDELEA UK. 8




## Wabunifu watafutiwa fursa SADC

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema itatumia kamati mbalimbali za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuwasaidia wabunifu katika sayansi na teknolojia ili wafanye utafiti kutatua changamoto ndani ya jamii.

Akizungumza katika maonyesho ya tisa ya Wanasayansi Chipukizi Tanzania (YST), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema kupitia Kamati ya Mawaziri wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wamejiwekea mipango ya kuendeleza wabunifu.

Alisema suala la kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu limepewa kipaumbele zaidi katika jumuiya hiyo inayoundwa na nchi 16.

"Kwa sasa, tumeweka mipango na taratibu kuwatambua wanasayansi na wabunifu, na jumuiya hii inaingia katika mapinduzi ya viwanda, hivyo kundi hili ni muhimu," alisema.

Prof. Ndalichako alisema maonyesho hayo yanaashiria elimu inayotolewa nchini inakidhi na kuwa na uwezo wa kutatua changamoto katika jamii.

Alisema amefurahi kuona miradi iliyoonyeshwa imeongezeka kutoka 81 na kufikia 95 ambayo ni mafanikio makubwa kwa sekta hiyo, huku idadi ya wasichana wanaoshiriki nayo ikiendelea kuongezeka.

"Najivunia kuona kuwa idadi ya wasichana imezidi kuongezeka na mwaka huu wasichana 88, sawa na asilimia 46, wameshiriki kuonesha ubunifu wao, naomba hii iwe chachu ya kuongeza idadi ya wasichana katika masomo ya sayansi," alisema.

"Zamani masomo ya sayansi hayakupendwa na wasichana lakini katika kipindi hiki kumekuwa na mwamko mkubwa na hii pia inachangiwa na jitihada za walimu katika uhamasishaji."

INAENDELEA UK. 8



Kijana akipanga matairi ili Katapila livuke bila kubomoa lami katika eneo la Tangi Bovu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Shehena vipodozi vyenye sumu yakamatwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ( TRA), limekamata katoni 230 za aina 11 tofauti ya vipodozi vyenye viambata vya sumu ambavyo vimepigwa marufuku kuingia nchini.

Vipodozi hivyo vilikuwa vikisafirishwa kwa njia ya magendo kwa kuchanganywa na mchanga wa shaba kutoka Zambia kwenda jijini Dar es Salaam.

Kukamatwa kwa shehena hiyo katika eneo la Chamwino katika, Manispaa ya Morogoro, barabara kuu ya Iringa-Morogoro, kumetokana na taarifa zilizopatikana kutoka kwa raia wema kwa polisi waliokuwa doria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kukamatwa kwa vipodozi hivyo Julai 30, mwaka huu, majira ya saa sita usiku, vikiwa kwenye maboksi yaliyoviringishwa karatasi za nailoni.

Mutafungwa alisema vipodozi hivyo vilikamatwa vikiwa kwenye lori lenye namba za usajili T 367 AXY aina ya Scania, mali ya kampuni ya usafirishaji ya Thornswift ya jijini Dar es Salaam.

"Walichofanya wasafirishaji ni kuchanganya maboksi haya yenye vipodozi vilivyopigwa marufuku na mchanga huo wa shaba uliokuwa kwenye kontena, ambao ulikuwa ukisafirishwa kutoka Zambia kwenda Dar es Salaam na baadaye China," alisema.

Akavitaja vipodozi vilivyokamatwa na kiasi cha katoni kwenye mabano kuwa ni Teint Clair (86), Bronze Tone Cream (31), Perfect White Cream (32), Perfect White Lotion (15) ,sabuni ya Perfect White (12), Carot Cream (18), Diana Lotion (12), Coco Pulp Cream (14), Actif Plus Cream (10) na Extra Clair katoni nane.

Aliwataja waliokamatwa wakihusishwa na tukio hilo kuwa ni dereva wa gari, Sudi Ally (60) mkazi wa Kongowe Mzinga jijini Dar es Salaam, ambaye awali inadaiwa alijaribu kutoroka na kulitelekeza lori hilo, lakini alitiwa mbaroni baada ya kufanyika msako, Samson Mhabe (22) dereva na mkazi wa Tunduma mkoani Songwe, ambaye alikuwa msindikizaji wa mzigo huo uliokamatwa.

"Watuhumiwa walidai vipodozi hivi walivipakia baada ya kuvuka mpaka wa Tunduma upande wa Tanzania na tunawashikilia pamoja na gari lililokamatwa likisafirisha bidhaa hizi kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa kushirikiana na TRA na TBS (Shirika la Viwango Tanzania)," alisema.

Meneja wa TRA Mkoa wa Morogoro, Emmanuel Maro, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Afrika Mashariki na Kati ya mwaka 2004, makosa katika ukamatwaji huo wa vipodozi, ikiwamo makosa kwa dereva na mmiliki wa gari, wanakabiliwa na makosa mawili.

Aliyataja makosa hayo kuwa ni kubeba na kusafirisha mzigo wa magendo ambao umezuiwa kinyume na kifungu namba 199 na kosa hilo ni faini isiyozidi Dola za Kimarekani 5,000.

Kosa lingine ni kuchezea muhuri wa pampu ya TRA kinyume cha sheria kwa sababu mzigo huo ulikuwa safarini ukitoka Zambia kwenda China lakini wao waliharibu muhuri uliofungwa na TRA mpakani na kuingiza mzigo huo wa magendo. Alisema kwa mujibu wa kifungu namba 195 cha sheria hiyo, faini yake haipungui Dola 2,500.

Maro akataja kosa la tatu kuwa ni mmiliki wa mzigo huo ambaye anakabiliwa na kosa la kuingiza mzigo uliozuiwa ambao adhabu yake ni kutoza ya asilimia 50 ya mzigo na kutaifisha na kwenda kuuteketeza kwa kushirikiana na TBS.


**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**

215227501



## HABARI KITAIFA

# Polisi yaonya wahalifu mkutano wa SADC

**Na Romana Mallya**

WAKATI Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akihamasisha kampeni ya usafi, Jeshi la Polisi limewaonya wahalifu kuelekea mkutano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Jumatatu, Makonda aliwataka wananchi wa mkoa wake kuwa wasafi wa miili yao na mazingira kuelekea mkutano huo mkubwa wa wakuu wa nchi 16 zinazounda jumuiya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo kutoka Makao Makuu ya Polisi, Liberatus Sabas, alisema wamejipanga na tayari wameanzisha operesheni maeneo mbalimbali kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama inaimarika wakati wote wa mkutano huo.

Mkutano huo umepangwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Agosti 17 na utahudhuriwa na wakuu wa nchi 16 wanachama.

Akizungumzia mkutano huo, Sabas alisema Jeshi la Polisi litahakikisha wageni wote wa mkutano huo watakuwa salama wakati wote wa mkutano na wanaondoka salama.

"Tumeanzisha operesheni maeneo mbalimbali kuhakikisha hali ya usalama inaimarika. Mikoa yote ambayo imepakana na Dar es Salaam na nchi kwa ujumla tutahakikisha inakuwa salama.

"Nitoe ujumbe kwa wahalifu, kama unafikiri hiki ni kipindi cha kujipatia, watajikuta wapo sehemu ambayo hawakuitegemea, watafute shughuli halali za kufanya wakati huu wa mkutano na siyo kujipanga kuja kujipatia vipato isivyo halali, wataishia mdomoni mwa simba.

"Ole wao watakaojaribu kwa maana tumejipanga vizuri, natoa rai kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa mbalimbali za matishio ya kihalifu, tunaahidi kwamba tutazifanyia kazi kwa haraka ili amani na utulivu uendelee," Sabas alisema.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vyingine vya ulinzi na usalama wamejipanga kikamilifu kuimarisha ulinzi.

**POLISI KILA KATA**

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi limewataka watendaji wa kata, wenyekiti wa serikali za mitaa pamoja na wananchi, kutoa ushirikiano kwa askari waliopelekwa kwenye kata zao ili kudumisha amani na utulivu nchini.

Sabas alisema katika kuimarisha hali ya ulinzi na usalama maeneo yote nchini, wameamua

INAENDELEA UK. 8

VisionFund TANZANIA

## TANGAZO LA MNADA

**VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LIMITED INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA INAKUSUDIA KUFANYA MNADA WA MALI ZA DHAMANA YA MIKOPO ILIYOWEKWA NA WATEJA WA BENKI KATIKA MIKOPO YAO HUSIKA. KUTOKANA NA WATEJA TAJWA HAPA CHINI KUWA WADAIWA SUGU, BENKI INATOA NOTISI YA MWISHO KABISA YA SIKU 14 KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI ILI WADAIWA HAWA WA BENKI WAWE WAMEKOMBOA DHAMANA ZAO KWA MUDA HUO. SIKU 14 ZIKIPITA BENKI ITAENDELEA NA ZOEZI LA KUUZA KWA MNADA MALI ZIFUATAZO ZA WADAIWA WAFUATAO:**

| JINA LA MDAIWA | MAHALI ILIPO | MALI YA DHAMANA |
|---|---|---|
| Kisiri, Ayubu Levava | Kakoy/Nkaiti/Arusha | Nyumba, Barua ya umiliki wa nyumba |
| Chembe, Gerald John | Babati | Shamba, Barua ya umiliki wa shamba |
| Lubuva, Mart M | Ndoroboni/Saraune/Magugu/Babati | Shamba,Uthibitisho wa Barua |
| Kayumbi, Capricon Conrad | Mpanzi/Mkali/Kalambo | Shamba, Uthibitisho wa ndugu |
| Luis, Samweli Sixtus | Myunga/Sumbawanga/Rukwa | |
| MWANISAW, HAGHAI VICENT | Myunga/mkali/Kalambo | Shamba ekari 30, uthibitisho wa umiliki wa shamba |
| Tenganamba,Vitus Geradi | Mikonko/kalambo | Shamba ekari 339.22, hati miliki ya Kimila ya shamba |
| Meli, Niko T | Matanga/Sumbawanga/Matanga | Shamba Ekari30, Barua ya tamko la mwenza wa muuzaji |
| Nasoro, Amor Hamis | Kamao/Sumbawanga/Rukwa | Toyota Wish station wagon,TV,SOFA,KABATI, Kadi ya gari na.: T490 DKM |
| Nassor, Suleiman Khamis | Karume/Sumbawanga/Rukwa | Gari-Mitsubish/fuso-T403 AUX, Kadi ya Gari |
| Msigwa, Hamisi I | Sumbawanga | Sem-Trailer-T925ADM, Kadi ya Trailer |
| Ngalawa, Charles D | Matai/Sumbawanga | Kiwanja Plot No. 62 Block, Hati ya Kiwanja |
| Anney, Aloyce Qambish | Tloma/Ganako/Karatu | Kiwanja, Uthibitisho wa Ndugu |
| Kunjumu, Pius Edward | Kinondoni/Daressalam | Gari Toyota hillux, Uthibitisho wa barua ya Mahakamani |
| Malley, Christian Mohe | Mkumbi/Orkesument/Simanjiro | Nyumba, Barua ya toleo la Kiwanja no.: 32 |
| Mpogolian, Salome | Loiborsireti/Kangala/Narakau | Shamba lenye Nyumba(ekari 50)&thamani za ndani, Hati ya Hakimiliki ya Kimila |
| KAZIULAYA, ROBERT DONALD | Kangala/Lobosiret/Lobosiret/Simanjiro | Shamba Ekari30,Uthibitisho wa shughuli ya kiuchumi ya Ndugu |
| Lazeri, Nemamiay S | Engonongoi-Terati | Shamba/Nyumba ekari 94.04, Hatiya Hakimiliki ya Kimila |
| Urassa, Godilisten Werandumi | Matadi/Ndumeti/Siha/Kilimanjoro | Kiwanja, Barua ya ufidiwaji wa shamba |
| Venance, Thomas Bizongwa | Ngarenairobi/Siha/Kilimanjaro | Kiwanja, Uthibitisho wa shughuli ya kiuchumi ya Ndugu |
| Saibogi, John Sunguye | Ngarenairobi/Siha/Kilimanjaro | Kiwanja Ekari20, Barua ya uthibitisho wa kumiliki kiwanja |
| Ngaisungui, Mokia M | Langai/Langai/Langai/Simanjiro | Shamba heka50, Fomu ya uthibitisho wa shughuli ya kiuchumi ya ndugu |
| Lekashu, Godwin M | Kimandulu/Arusha | Gari-toyota double cabin-pick up T241AFL. TV,Radio,Kabiti,Jiko, Kadi ya Gari |
| Ndipoyi, Kordoni P | Ilchalai/narakau/loiborsiret/erkasument | shamba,Uthibitisho wa Umiliki wa Shamba |
| Kipaley, Bahati Lorikuta | Olndotop/Narakauwo/Loibor-siret/Simanjiro | Shamba hekari20, Barua ya uthibitisho wa kumiliki Shamba |
| Munga, Yusuph Mohamed | Lobosireti/Kangala/Simanjiro | Shamba Ekari 169.35&Ng'ombe 20, Hati yaHakimiliki ya Kimila |
| DAU, HAMISI RAMADHANI | Lolkisale/Lolkisale/Monduli | Nyumba, Fomu ya uthibithso wa umiliki |
| LAIZER, ELIYA NANGAN | Lashaine/Monduli | Nyumba,Shamba(ekari 4),pikipiki, Mkataba wa kuuziana Kiwanja ya tarehe 15 Juni 2008 |
| LAIZER, SOLOMON OLEMUTETI | Sepeko/Lashaine/Lahaine/Monduli | Shamba Ekari82, Hati ya hakimiliki ya kimila |
| Kashiro, Gerald | Ingug/Emboreer/Simanjiro | Shamba, Uthibitisho wa barua |
| Auto, Kassim Issa | Mirongoine/Kigongoni/Oljoro | Nyumba, Hati ya Hakimiliki ya Kimilia |
| Mollel, Lucas Zakaria | Emboreet/Emboreet/Simanjiro | Shamba, Barua ya utambulisho |
| MPUME, BASHIRI RAMADHAN | Nia/Lolkisale/Lolkisale/Monduli | Shamba 15, Hati ya haki miliki ya kimila no.: 072 |
| Lenjala, Mathayo Noah | Engonongo/Terat/Orkasment | Shamba Ekari 39.65, Hati ya hakimiliki ta kimila no.: 072 |
| Shekidele, Morrice Thadey | Lobosioit/Emboretr | Shamba ekari 50, Uthibitisho wakubalidishwa eneo kwa sabsbu ya migogoro ya Kijiji |
| KURESOY, PARANA KURESOY | Enguiki/Enguiki/Arusha | Shamba, Uthibitisho wa shughuli ya kiuchumi ya Ndugu |
| SAITOTI, ZAKAYO LEIYAN | Lashine/LokisaleMonduli | Kiwanja&Ng'ombe(15), Fomu ya uthibitisho wa shamba |
| Mollel, Jackson O | Langai/Langai/Langai/Simanjiro | Shamba Heka30, Fomu ya uthibitisho wa shughuli ya kiuchumi ya ndugu |
| Siria, Shilalo O | Nadunjuki/Komolo/Simanjiro | Shamba/Ngombe 200, Fomu ya uthibitisho wa shamba |
| Nokoyo, Bahati N | Langai/Erkasument/Simanjiro | Kiwanja ekari 0.5, Uthibitisho wa Kupewa Kiwanja no.:20 |
| Kelele, Noah Lengoje | Orikiringo/Narakau/Loborsiret / Orkasment | Shamba heka50,Barua ya Kibali cha Umiliki wa Shamba |
| Mollel, Michael L | Narakauwo/Narakauwo/Loibosiret/Orkasument | Shamba Ekari60, Barua ya uthibitisho wa kuwa na shamba ekari 60 |
| Mollel, James M | Simanjiro | Shamab ekari 99, Hati ya umiliki wa shamba |
| Nginaani, Naata Mberekeri | Lendikinya/Monduli | Shamba( Ekari 150), Barua ya Kijiji ya Umiliki wa Shamba |
| MOLLEL, MESARIEKI NAURELUMBWA | Lokisale-Monduli | Nyumba, Kibali cha Umiliki wa Ardhi Kum S/K/LO/KIBAL/MD/0049 |
| LAIZER, MATHAYO FARU | Ndotoi/Naraku/Lobosireti/Simanjiro | Shamba ekari 40, Hati ya umiliki wa shamba ya tarehe 25 Mei 2016 |
| LAIZER, JULIUS SIGILE | Langai/Erkasument/Simanjiro | Shamba ekari 70, Uthibitisho wa Umiliki wa Shamba |
| MAKUNGU, CAROLINE DANFORD | Kangala/Lobosiret/Lobosiret / Simanjiro | Kiwanda, Hati ya kumiliki shamba Kijiji cha Loiboirsiret |
| TINGAROI, JULIUS NDORESI | Narakauwo/Lobosiret/Orkesment | Shamba na Kiwanja, Uthibitisho wa hati halali ya shamba |
| YONATHAN, TABITHA YONATHAN | Loiborsiret/Loborsireti/Orkesment | Shamba ekari 17, Uthibitisho wa Shamba la Aloice Pita |

215358602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars kazeni buti Harambee inafungika

**KESHO** Taifa Stars itashuka uwanjani ugenini nchini Kenya kuivaa timu ya Taifa hilo, Harambee Stars, kwenye mechi ya marudiano ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Taifa Stars itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare tasa na Harambee Stars katika mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa Taifa Jumapili iliyopita.

Kwa matokeo hayo, Stars sasa inahitaji ushindi ama sare yoyote ya mabao ili kuweza kusonga mbele katika michuano hiyo itakayofanyika mwakani nchini Cameroon.

Timu itakayopata matokeo kwenye mechi hiyo ya kesho itakutana na mshindi wa jumla kati ya Sudan Kusini ama Burundi ambayo katika mechi ya awali ikiwa nyumbani ilishinda 2-0.

Kwa ujumla tunaimani kubwa na kikosi hicho cha Stars chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Mrundi Etienne Ndayiragije akisaidiwa kwa karibu na wazawa Selemani Matola pamoja na Juma Mgunda.

Hiyo ni kutokana na namna ambavyo Taifa Stars ilivyocheza na kufanikiwa kumiliki mpira kwa asilimia kubwa zaidi ya Harambee Stars katika mechi ya awali ikiwa ni baada ya Ndayiragije na wasaidizi wake kuanza kukinoa kikosi hicho kwa muda mfupi mara baada ya kuteuliwa kukinoa katikati ya mwezi uliopita.

Kwa namna ambavyo Stars ilicheza mechi ya awali, ilionyesha kukamilika idara zote, lakini makosa madogo madogo katika safu ya ushambuliaji na viungo wa kati kushindwa kuelewana vizuri, yanaweza kuwa chanzo cha kukosa ushindi kwenye mchezo wa awali.

Kwa kuwa hiyo ilikuwa ni mechi ya kwanza kabisa kwa Ndayiragije na wasaidizi wake kukiongoza kikosi hicho, tunaimani amegundua makosa yaliyojitokeza na tayari ameyafanyia kazi kuelekea mechi hiyo ya kesho ugenini.

Lakini pia ari na hamasa kutoka kwa wachezaji ni baadhi ya mambo ambayo yanatupa imani kwa Taifa Stars kupata matokeo na kusonga mbele hatimaye kufuzu michuano hiyo kwa mara ya pili tangu ilipoanzishwa mwaka 2009.

Tunatambua si rahisi kupata ushindi kwa Harambee Stars ikiwa nyumbani huku ikiwa na kocha wake, Mfaransa Sebastien Migne ambaye wamekuwa naye kwa muda mrefu sasa, lakini kama wachezaji watakaza buti huku wote wakiwa na nia moja tu ya ushindi, tunaamini Taifa Stars inaweza kupata matokeo na kuwashangaza wengi ambao wanaamini haiwezekani.

Kinachotakiwa kwa wachezaji wa Stars ni kuondoa woga wa kucheza ugenini na kujiona kama wapo uwanja wa nyumbani na kupambana mwanzo mwisho bila uoga wowote.


Tunatambua Harambee Stars watakuwa 12 uwanjani kwa maana ya mashabiki wao jukwaani ambao jukumu lao litakuwa moja tu kuwapa hamasa wachezaji wao 11 dimbani kuwashangilia mwanzo mwisho, lakini hilo haliwezi kuwa sababu kwetu kukataa tamaa ya kupata matokeo.

Taifa Stars inaundwa na wachezaji wengi walioshiriki michuano ya Afcon mwaka huu nchini Misri ukilinganisha na Harambee Stars, hivyo uzoefu walioupata katika fainali hizo, tunaamini watautumia vema wakiwa ugenini kuweza kupata matokeo kwa kuwa si mara yao ya kwanza kucheza mechi ya kiushindani ugenini. Nipashe kama ilivyo kwa wadau wengi wa soka nchini, tunatamani kuona Stars ikifuzu fainali hizo na Watanzania kuanza kujiandaa kwa safari ya kwenda Cameroon kuiunga mkono kama ambavyo hamasa ilivyokuwa katika fainali za Afcon 2019 nchini Misri.

Tunaitakia kila la kheri Taifa Stars wakati huu tukiamini huu ni mwaka wa Tanzania kufanya vizuri kimataifa kwa kufuzu fainali hizo baada ya mwaka huu kutimiza lengo la awali la kufuzu na kushiriki Afcon kwa mara ya pili katika historia ya Tanzania kwenye michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Maneno ni kama fumo ...

**HUSEMWA** "Maneno ni kama fumo, yakitoka mdomoni hayarudi." Maana yake neno analotamka mtu ni kama mkuki (fumo), likitoka halirudi na huweza kuleta madhara.

Twanasihiwa tuwe na tabia ya kuyatafakari maneno tuyasemayo. Ni vizuri kulipima neno kabla ya kulisema na kujiletea majuto baadaye.

"Hadhari kabla ya hatari" maana yake ni vizuri kutahadhari kabla ya kufanya jambo tusije kufikwa na hatari au maangamizo. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na hadhari kabla ya kutenda mambo. Aidha, yatufunza tusiwe na tabia ya kudakia mambo bila ya tahadhari.

"Poteza" ni kitendo cha kusababisha kitu kuwa mahali kisipoonekana; sababisha kitu kipotee; pia tumia wakati vibaya. Hapa twapata potezana, potezea, potezeana, potezesha, potezewa na potezwa.

Gazeti fulani la michezo liliandika: "Kakolanya: Nitampoteza vibaya Manula." Kichwa cha habari hiyo kilinishitua na kufanya nisome kwa makini ili nipate maana yake. Paragrafu ya nane kati ya 12 ndiyo iliyonivutia zaidi. Aliongeza (Kakolanya): "Yanga nilikuwa namba moja, sikuwa napata ushindani, kitu ambacho kilinifanya nione nipo bora, kumbe nilijidanganya, lakini uwapo wa Manula Simba, utanifanya nipambane zaidi ili niwe bora zaidi na kumpora namba."

Ukurasa wa mbele wa gazeti hilo kuna picha ya Kakolanya akitia saini kuthibitisha sasa ni mchezaji halali wa Simba. Chini ya picha hiyo kuna maneno haya: "Kakolanya: Nitampoteza vibaya Manula."

Hapa ndipo paliponishitua. Mbona paragrafu zote 12 sikuona mstari wowote ulioandikwa Kakolanya kasema "Nitampoteza vibaya Manula?" Kama ndivyo, Kakolanya ana maana gani kusema "atampoteza vibaya Manula?" Maana ya 'poteza' ni kitendo cha kusababisha kitu kuwa mahali kusipoonekana. Maana ya 'vibaya' ni kisichokuwa katika hali nzuri.

Kama ni maneno ya mwandishi, yaweza kuleta chuki kati ya Kakolanya na Manula; kila mmoja kudhani mwenziye ni mshirikina anayetaka kumnyang'anya tonge mdomoni!

Hata hivyo, katika paragrafu ya tisa Kakolanya alinukuliwa kusema: "Yanga nilikuwa namba moja, sikuwa napata ushindani, kitu ambacho kilinifanya nione niko bora, kumbe nilijidanganya, lakini uwapo wa Manula Simba utanifanya nipambane zaidi ili niwe bora zaidi na kumpora namba." Maneno ya "Nitampoteza vibaya Manula" yalitokea wapi?

"Hadhari kabla ya hatari." Ni vizuri kutahadhari kabla ya kufanya jambo tusije kufikwa na hatari au maangamizo. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuwa na hadhari kabla ya kutenda mambo. Tusiwe na tabia ya kudakia mambo bila ya tahadhari. Tuandike maneno yanayotamkwa na msemaji bila kuongeza yetu au kutia chumvi. Ni kumtilia mdomoni maneno ambayo msemaji hakuyasema!

'Chama' ni neno lenye maana tatu lakini nitaeleza moja tu ambayo ni muungano wa watu wenye lengo moja. Kundi lenye kufuata kaida au silka fulani zenye kuegemea dini, siasa, misimamo ya jamii, uchumi, michezo au jambo lingine lolote lenye maazimio maalumu.

Kila mkoa nchini una vyama vinavyosimamia maendeleo ya mchezo wa kandanda, navyo vipo chini ya uangalizi wa Shirikisho la Vyama vya Kandanda nchini, TFF. Hata hivyo Shirikisho hilo limejikita zaidi kwenye klabu zinazoshiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara, hasa Simba na Yanga!

Yanga walikuwa na shughuli maalumu iliyoitwa 'Kubwa Kuliko' (kuliko nini?) kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam. Lengo lilikuwa kupata shilingi bilioni 1.5 zitakazowasaidia kufanya usajili mzuri msimu ujao.

Kilichoshangaza wengi ni kutoonekana kiongozi yeyote wa juu wa TFF, ingawa walialikwa! Badala yake shirikisho hilo liliwakilishwa na Mwenyekiti wake wa Kamati ya Uchaguzi, Ally Mchungahela, jambo lililowahuzunisha wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga.

Yakatokea manung'uniko na malalamiko miongoni mwa waliokuwapo, wakisema hata Iftar iliyoandaliwa na klabu hiyo kwenye Hoteli ya Serena wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, viongozi wa TFF hawakuhudhuria, ingawa walialikwa! Kuna madai kuwa Simba ilipowaalika viongozi hao kushiriki Iftar walihudhuria. Hali hii yaleta picha gani kwa wanachama, wapenzi na mashabiki wa Yanga kuona baba mmoja (TFF) akiwabagua wanawe? Nadhani hii ndio sababu iliyomfanya Rais mstafu wa awamu ya nne, Jakaya Mrisho Kikwete kuwanasihi viongozi mbalimbali wa kandanda nchini kufanya uamuzi wa usawa bila kujali timu wanazozipenda.

Pia alizitaka klabu kubadilika ili kuwaendeleza vijana na wachezaji wazawa badala ya kuwajenga wachezaji wa kigeni wasiokuwa na faida kwa Tanzania.

"Chako ni chako, cha mwenzako sio chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Methali hii yatufunza umuhimu wa kuvitegemea vitu vyetu kuliko vya wengine. Kinachoishinda TFF kuwa na chuo maalum cha kukuza vipaji vya vijana watakaokuwa wawakilishi wetu kwenye michezo ya kimataifa ni kitu gani?

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Waziri aagiza mwekezaji apewe leseni

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamampori Tanzania (Tawa), kumpatia leseni ya muda mwekezaji mzawa anayemiliki bustani ya wanyamapori ya Bahari iliyoko Tegeta, jijini Dar es Salaam ili aendelee kuwahudumia Wanyamapori hao.

Kanyasu ametoa agizo hilo kutokana na Tawa kumnyima mwekezaji huyo kwa miaka miwili sasa kwa madai kuwa ameshindwa kuwatunza ipasavyo wanyamapori hao.

Akizungumza jana baada ya ziara katika Bustani ya Wanyamapori ya Bahari (Bahari Zoo), Kanyasu aliagiza Tawa kutuma wataalam mara moja katika bustani hiyo kwa ajili ya kushughulikia suala hilo.

Kitendo hicho cha kumnyima leseni tangu mwaka 2017 na kutokumnyang'anya wanyamapori aliokuwa nao na kushindwa kumpa maagizo yoyote, mwekezaji huyo ameendelea kubaki nao hadi sasa, hivyo Kanyasu kuiagiza Tawa ipitie upya uamuzi wake kama una tija kwenye uhifadhi.

"Mtu mnamnyang'anya leseni ya kuendesha biashara halafu mnamwachia wanyama ambao mnadai ameshindwa kuwatunza. Hii maana yake nini?" alihoji Kanyasu.

Alisema kitendo hicho kimeikosesha serikali mapato kwa vile mwekezaji huyo katika kipindi chote alichonyimwa leseni ameshindwa kulipa kodi kwa kwa vile hana leseni ya kuendeshea biashara hiyo.

Naibu Waziri alisema hatua hiyo inapingana na maelekezo ya serikali aliyoyatoa bungeni hivi karibuni ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika biashara ya bustani za wanyamapori baada ya serikali kupiga marufuku kusafirisha nje wanyamapori hai.

Mmiliki wa bustani huyo, Willy Kussaga, alisema kitendo cha kunyimwa leseni kimechochewa na wafanyabiashara wenzake wanaofanya biashara kama hiyo.

Kusaga alimweleza Naibu Waziri kuwa alishamuandikia barua Rais John Magufuli ili alishughulikie suala hilo.

Pia alisema tangu serikali ipige marufuku kusafirisha wanyamapori hao, kitendo hicho kimewagharimu sana kwa vile ilisimamisha ghafla hali iliyosababisha wafugaji hao kuyumba kiuchumi.

Amesema tangu kunyimwa leseni ameendelea kuwalisha wanyamapori hao jambo ambalo ni gharama kubwa sana.

"Hapa tuna simba wawili pamoja wanyama wengine ambao kuwatunza hawa ni gharama zaidi. Tunamwomba Rais atusaidie ili tuendelee na shughuli hii," alisema.



Mkuu wa shule ya sekondari Pius, iliyoko Kongowe Mbagala, jijini Dar es Salaam, Stephen Haruna (kushoto), akimkabidhi zawadi mwanafunzi aliyemaliza kidato cha sita, Benard Deogatius kwa niaba ya wanafunzi wenzake, shuleni hapo, jana, baada ya shule hiyo kufaulisha daraja la kwanza na la pili pekee kwenye matokeo ya kidato cha sita mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule yataja siri kuwabwaga wakongwe

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari ya Patrick Mission, iliyoko Madale jijini Dar es Salaam, ambayo katika matokeo ya kidato cha sita hivi karibuni ilifaulisha wanafunzi wake wote kwa daraja la kwanza na la pili, imetaja sababu ya kuzibwaga shule kongwe kitaifa.

Mkuu wa shule hiyo, Cletus Kilamba, alisema jana kuwa wameyapokea matokeo hayo kwa furaha kubwa kwa kuwa shule hiyo imekuwa miongoni mwa shule nne pekee za Dar es Salaam zilizoingia 20 bora kitaifa. Alisema kwenye matokeo hayo, wanafunzi 37 waliohitimu kidato cha sita walipata daraja la kwanza na 21 daraja la pili na hakuna mwanafunzi aliyepata kuanzia daraja la tatu hadi sifuri.

"Kuna shule kubwa ambazo mara nyingi zinaingia 20 bora kitaifa lakini sisi mwaka huu tumekuwa miongoni mwa shule nne pekee za Dar es Salaam zilizoingia 20 bora kitaifa kwa hiyo tuna kila sababu ya kufurahia matokeo ya mwaka huu," alisema

Kilamba alisema shule hiyo imekuwa na kawaida ya kuchukua wanafunzi wenye uelewa wa aina tofauti hata wale wenye uelewa mdogo na kisha huwaandaa vyema na katika mazingira mazuri kwa ajili ya mitihani ya kitaifa na mwishowe hufanya vyema.

Alisema hata kwenye matokeo ya kidato cha pili na cha nne, wamekuwa wakifaulisha wanafunzi wengi kwa daraja la kwanza na la pili kutokana na jitihada kubwa inayofanywa na walimu na uongozi wa shule hiyo.

"Tunawapongeza sana walimu wetu kwa namna wanavyotupa ushirikiano mkubwa kuhakikisha shule yetu inaendelea kuwa juu mwaka hadi mwaka, tunawaomba waendelee kutupa ushirikiano kama huo ili Patrick Mission iendelee kuwa juu mwaka hadi mwaka," alisema

"Kwa matokeo haya tunaomba wazazi watuamini watuletee watoto wao tuwalee hapa Patrick Mission kwani kuna michepuo mingi, mazingira mazuri ya kusomea na nawahakikishia wazazi hawatajuta kuwaleta watoto wao maana tutahakikisha wanafaulu kwa madaraja ya juu."

Alisema kuna mambo mengi yamechangia matokeo mazuri kama hayo ikiwamo mazingira bora ya kufundishia yaliyowekwa na uongozi wa shule kwa walimu na wanafunzi ikiwamo maabara na maktaba za kisasa za shule hiyo.

## Kigogo Tigo kortini kutakatisha fedha

**Na Hellen Mwango**

WATU 10 wakiwamo wafanyakazi watatu wa kampuni ya Simu za Mkononi ya Tigo, na kigogo wa kampuni hiyo, Hamis Singa (30), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa kesi mbili za uhujumu uchumi.

Kesi hizo ni pamoja ni kula njama, kujipatia fedha na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 48, kupitia ujumbe mfupi wa 'tuma kwenye namba hii'.

Mbali na Singa, washtakiwa wengine ni wakulima wakazi wa mkoa wa Manyara na jijini Arusha, Jailos Joseph (33), Jonas Mnunga (32), Japhet Mkumbo (33) na Omari Omari (33).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Salum Ally.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa siku na mahali pasipofahamika kati ya Januari na Julai, mwaka huu, katika mikoa ya Manyara, Arusha na sehemu mbalimbali nchini, washtakiwa walikula njama ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa kati ya Januari na Julai, mwaka huu, katika mikoa ya Manyara, Arusha na mingine, kwa njia ya udanganyifu, washtakiwa wote walijipatia Sh. 26,432,441 kupitia huduma kwa wateja wa mitandao ya Vodacom na Airtel.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa mwezi, mwaka na mahali pa shtaka la pili, washtakiwa wote kwa pamoja walisambaza ujumbe mfupi wa simu ya mkononi kwamba 'Tuma pesa kwenye namba hii' huku wakijua ni kinyume cha sheria.

Shtaka la nne na tano, ilidaiwa kuwa mwezi, mwaka na mahali pa shtaka la pili, washtakiwa wote walisambaza ujumbe mfupi ulipo shtaka la tatu kwenye simu za watu tofauti kwa lengo la kujipatia fedha. Shtaka la sita, linamkabili kigogo huyo wa kampuni ya Tigo, Singa, Babati mkoani Manyara kuwa aliingilia miamala ya fedha ya mawakala wa Tigo kwa lengo la kujipatia fedha.

Katika shtaka la saba, ilidaiwa kuwa kati ya Januari na Julai, mwaka huu, katika mikoa ya Manyara, Arusha na mingine nchini, washtakiwa walitakatisha Sh. milioni 26.4 huku wakijua zimepatikana kwa njia ya udanganyifu.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu aliagiza washtakiwa wapelekwe mahabusu mpaka Agosti 15,mwaka huu.

Wakati huohuo, watu wengine watano, Mohammed Abdallah (25), Mosses Kilosa (29), Ofisa wa Huduma kwa Wateja Tigo, Tawi la Mlimani City, Kokubelwa Karashani (35), Wakala wa Tigo, Godfrey Magoye (30) na mfanyakazi wa Tigo, Khalfani Milao (29), wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kuingilia miamala ya fedha na kujipatia zaidi ya Sh. milioni 20.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile.

Wankyo alidai kuwa washtakiwa hao waliingilia miamala ya fedha ya watu tofauti na kujipatia Sh. 20, 378,627.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao walitakatisha zaidi ya Sh. milioni 20.3 baada ya kujipatia kwa njia ya udanganyifu.

# MO kuwekeza kumwaga ajira 100,000

INATOKA UK. 2

huo utalenga kwenye viwanda vya kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngano na mahindi ikiwamo kiwanda cha kutengeneza biskuti, tambi na bidhaa nyingine kwa lengo la kuongeza thamani ya mazao nchini.

"Nikudokezee pia kuwa, kutokana na uongozi wako na hatua thabiti ulizochukua kwenye sekta ya sukari nchini, tumeshawishika kuwekeza kwenye kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari.

"Lengo ni kuhama kutoka kwenye biashara ya kuagiza sukari na kuwa wazalishaji wa sukari kuitikia wito wako wa kutatua tatizo la sukari nchini ambapo tunatarajia kuwekeza Sh. bilioni 340.

"Tunatarajia pia kuwekeza kwenye nyanja ya mawasiliano, mafuta na miundombinu ya bandari ya nchikavu. Kwa ujumla, tunatarajia kuwekeza Sh. bilioni 860 na kuongeza ajira kutoka waajiriwa 30,000 kwa sasa hadi kufikia waajiriwa 100,000 mnamo mwaka 2025.

"Sisi Mohammed Enterprises tumekuwapo katika biashara hapa nchini kwa miaka 50 sasa. Tutaendelea kuwekeza hapahapa. Habari nzuri zaidi ni kwamba, hapa nyumbani kunazidi kunoga chini ya uongozi wako madhubuti. Natumia fursa hii kuwaambia wawekezaji wa nje na Watanzania wenzangu kuwa waje Tanzania kumenoga," MO alisema.

**AMPONGEZA JPM**

MO pia alimpongeza Rais Magufuli kwa uongozi mzuri na hatua anazozichukua za kukuza na kujenga uchumi wa nchi, akieleza kuwa ameshuhudia mageuzi makubwa katika kipindi kifupi.

"Katika historia ya nchi yetu, baadhi yetu tumekuelewa mapema sana, tuna uhakika kabisa wale wasiokuelewa sasa, watakuelewa tu baadaye. Wasioelewa lengo, wataeleweshwa na matokeo ambayo tunaamini hayako mbali sana.

"Mageuzi haya makubwa chini ya uongozi wako ndiyo yaliyotushawishi kuendelea kuwekeza nchini kama unavyoshuhudia leo hii. Binafsi nashuhudia kuimarika kwa nidhamu kwa watumishi wa umma, mkazo mkubwa serikali uko kwetu sisi wawekezaji wa ndani, kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo, kupungua kwa rushwa na kushughulikiwa kwa migogoro ya ardhi nchini.

"Tumeguswa na namna ulivyoshughulikia matatizo ya wafanyabiashara katika mkutano wako na wafanyabiashara na tumefurahishwa na utayari ulioonyeshwa wa utekelezaji wa BluePrint kutokana na mabadiliko ya kisheria yaliyofanyika katika kikao cha Bunge la Bajeti lililopita," MO alisifu.

Mfanyabiashara huyo pia alimpongeza Rais Magufuli na serikali yake kwa uwekezaji unaofanywa kwenye reli, usafiri wa anga, umeme na barabara, akieleza kuwa kukamilika kwa miradi hiyo kutapunguza bei za bidhaa zinazozalishwa na kampuni zake.

Rais Mgufuli alimpongeza MO kwa uwekezaji wake na kueleza kuwa kila anapopata mwaliko wa kufungua kiwanda, hufurahi kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya uchumi wa nchi yoyote.

Alisema serikali inaipenda na inaithamini sekta binafsi kwa kuwa ndiyo injini ya uchumi wa nchi na inaongoza kwa kutoa ajira kwa wananchi.

Rais Magufuli alisema kutokana na ukweli huo, serikali yake imefanya jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufuta kodi 54 zilizokuwa kero, kuhakikisha kunakuwa na umeme wa uhakika na ujenzi wa miundombinu ili kuwe na ustawi wa sekta hiyo.

"Nawaambia kwa dhati kabisa serikali hii ipo kwa ajili ya wawekezaji, serikali hii ipo kwa ajili ya sekta binafsi, nchi yoyote haiwezi kusonga bila sekta binafsi, nchi yoyote haiwezi kufanya biashara, biashara inafanywa na sekta binafsi.

"Mwajiri mkubwa wa watanzania ni sekta binafsi, haiwezi kuwa serikali, serikali haina uwezo wa kumwajiri kila mtu, tuko milioni 55 lakini ni sekta binafsi ndiyo inaweza kuajiri watu wengi," alisema.

# Wabunifu watafutiwa fursa SADC

INATOKA UK. 4

Aliwaomba walimu kuwafundisha wanafunzi kufanya utafiti ambao utasaidia ukuaji wa uchumi hasa katika mapinduzi ya viwanda.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (Costech), Dk. Amos Nundu, alisema kwa muda mfupi, vijana kupitia YST wamefanya utafiti ambao ukiendelezwa utaleta mabadiliko chanya katika taifa na ujenzi wa viwanda.

"Mfumo huu ni mzuri kwa kuwa unasaidia kwajenga vijana wadogo wenye uwezo wa kufanya utafiti wenye weledi unaosaidia kuchangia ukuaji wa uchumi wa viwanda," alisema.

Mwanzilishi Mwenza wa YST, Dk. Gosbert Kamugisha, aliwapongeza washiriki na kuiomba serikali kuendeleza kazi zao za kibunifu.

Katika maonesho hayo, washindi walikabidhiwa vikombe, medali na fedha taslimu, huku mshindi wa jumla wa ubunifu akitoka katika Shule ya Sekondari ya Chief Dodo iliyoko mkoani Manyara, ubunifu ukiwa umefanywa na wanafunzi wawili, Editha Philipo (kidato cha tatu) na Nasra Mpochi (kidato cha nne).

# Lugola awakingia kifua bodaboda

INATOKA UK. 3

hivyo huku askari wa usalama barabarani wakiwa wamewapanga wawapo maeneo husika.

"Mheshimiwa Lugola, tunaamini kabisa leo kero zetu zinaisha kabisa, sisi malalamiko yetu ni kwa Sumatra na halmsahuri hawatutendei haki, wanatupa kero, tunashindwa kuifanya kazi hii kwa furaha kutokana na faini zao pamoja na kutuhamisha maeneo mara kwa mara," alisema mwendesha bodaboda aliyejitambulisha kwa jina la Fikiri Bathromeo.

Lugola aliwataka polisi mkoani humo kutowanyanyasa waendesha bodaboda kwa kuwa Rais John Magufuli anataka wafanye kazi kwa amani huku wakifuata sheria.

"Kuwachezea hawa ni sawa kuchezea mboni ya Rais John Pombe Magufuli, wawekeeni utaratibu, hakika watatii, leo mnawaambia hivi, kesho mnawahamishia kule, hapo kosa siyo lao, bali ni lenu," alisema.

Aliongeza kuwa ameagiza utaratibu uwekwe na Jeshi la Polisi kuhusu wapi wawapo na si wasumbuliwe.

"Naagiza wote waliovunja utaratibu wa maegesho ya bodaboda na bajaj hizi wakamatwe maana utaratibu uliwekwa, lakini wapo wajuaji wakabadili mfumo wa maegesho hayo, hii haiwezi kuvumilika hata kidogo," alisema.

Mkutano huo uliandaliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro na kumwalika Waziri Lugola ili kutatua kero zinazolikabili kundi hilo.

Wamiliki na waendesha bajaj na bodaboda takribani 1,000 walishiriki mkutano huo na wengi wao walipata nafasi ya kumuuliza waziri huyo maswali mbalimbali.




Dereva wa bodaboda akiwa amembeba abiria mtoto bila kofia ngumu kwa ajili ya usalama, eneo la Kimara Baruti, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo ambacho ni kinyume na sheria za usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Polisi yaonya wahalifu mkutano wa SADC

INATOKA UK. 5

kupeleka askari kwenye kata zote ili kuhakikisha huduma ya polisi inawafikia wananchi kwa karibu.

"Tunaomba wapewe ushirikiano ili wasaidie kutatua kero mbalimbali za uhalifu na wahalifu," alisema.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, Sabas alisema wamejipanga kuhakikisha unafanyika kwa amani na utulivu na atakayeivunja atashughulikiwa.

"Hakuna watu wasiojuliana, watu wasiojulikana hawapo, suala ni kwamba tukio linapotokea huyo mtu anakuwa hajajulikana, uchunguzi unavyoendelea mhusika anajulikana," Sabas alisema baada ya kuulizwa kuhusu changamoto ya watu kutekwa na watu wanaoitwa 'wasiojulikana'.

"Taratibu za uchunguzi siyo lazima uishe mwezi mmoja, miwili au mitatu ndiyo maana sheria inasema jinai haiishi, hakuna kipindi cha kumaliza jinai, unaweza kupeleleza baada ya mwaka, miaka miwili, mitatu au minne, hili ni suala la muda.

"Hakuna usugu kwenye matukio haya, hayo ni maneno yanayoibuka mitaani lakini kama mtuhumiwa hajapatikana ni mambo ya kawaida, atatafutwa na baada ya muda atapatikana na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Watu wasiojulikana ni maneno ya mitaani," alisema.

# CUF yaipima ubavu polisi

INATOKA UK. 3

kuwahamasisha kushiriki katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Kambaya aliwataja viongozi wengine watakaohudhuria katika mkutano huo kuwa ni wakurugenzi wa chama hicho, Mneke Jaafar, Mohammed Ngulangwa na Salvatory Magafu.


Mkutano huo umepangwa kufanyika kukiwa na zuio kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara isipokuwa kwa wabunge, madiwani na wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji katika maeneo yao.

Julai 9, mwaka huu, Jaji Mutungi alikaririwa akisema hajawahi kupokea malalamiko ya kimaandishi ya vyama vya siasa kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara.

Januari 27, 2001 kisiwani Pemba, CUF ilifanya maandamano na kusababisha Jeshi la Polisi kufyatua risasi kwa waandamanaji na baadhi yao kupoteza maisha akiwamo askari polisi.

Mapema wiki, akiwa Unguja, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliwakumbusha polisi kuhusu kusimamia zuio la mikutano ya kisiasa na maandamano, akieleza kushangazwa kwake kuona mwanachama mpya wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, anafanya mikutano kisiwani huko bila kuchukuliwa hatua.

Alisema ameshangaa kuona Jeshi la Polisi halichukui hatua dhidi ya Maalim Seif ilhali kiongozi huyo wa zamani wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sasa si kiongozi wa kuchaguliwa katika eneo lolote nchini.



# Hakimu mshitakiwa alalamika kortini

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WASHITAKIWA watano, akiwamo Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Bernad Nganga, wanaokabiliwa na makosa 11 katika kesi ya utakatishaji fedha haramu na uhujumu uchumi, wamelalamika kuchelewa kwa upelelezi wa kesi yao.

Kutokana na madai hayo, washtakiwa hao jana waliwasilisha hoja zao kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, kuiomba kufuta makosa yote ambayo upelelezi ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 60 na kubaki na kosa moja la kughushi ambalo halina ukomo wa upelelezi.

Washitakiwa wengine katika kesi hiyo ni mwanasheria wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Maneno Mbunda, Nelson Kangero, Wakili wa Serikali Mkoa wa Arusha, Fortunatus Mhalila na Tumaini Mdee.

Hoja hizo ziliwasilishwa mahakamani hapo kwa niaba ya washitakiwa hao na mawakili wa utetezi, Elibariki Maeda, Valentine Nyalu na Fridolin Bwemelo.

Walidai kuwa upande wa mashtaka umechelewesha upelelezi kwa zaidi ya miezi miwili, hivyo ni vyema uelekezwe kuanza kusikiliza kesi yao na kama upelelezi bado, upande wa mashitaka uiondoe kesi hiyo mahakamani kwa kuwa waliifungua kinyume cha notisi ya serikali.

Walidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umechukua muda mrefu na kwenda kinyume cha notisi namba 296/2012 ya Serikali iliyohimiza kesi zisifunguliwe kabla ya upelelezi kukamilika.

Aidha, walidai kuwa washitakiwa hao wamekaa ndani zaidi ya siku 60 sasa na watatu kati yao ni watumishi wa serikali na wanaendelea kulipwa mshahara na huku wakila chakula cha bure gerezani bila kuzalisha na kuipa serikali hasara mara mbili.

Kadhalika, walidai kuwa makosa mengi yaliyo kwenye hati ya mashitaka yalipaswa kukamilika ndani ya miezi miwili.

Walidai kuwa shauri hilo lilipofikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza, wakili wa serikali alidai kuwa upelelezi uko ukingoni jambo walilohoji iweje mpaka sasa zaidi ya miezi miwili haujakamilika.

"Hili wanaenda kinyume cha maelekezo ya Rais John Magufuli aliyoyatoa alipotembelea gereza la Butimba, Mwanza.

Aliagiza upelelezi ufanyike haraka ili watu wapungue magerezani. Tunaiomba mahakama imuunge mkono mheshimiwa Rais kwani amesema hataki kuongoza nchi ya watu wanaonung'unika na wanaolia machozi," alidai Wakili Maeda.

Baada ya hoja hizo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Niku Mwakatobe, alisema hoja walizotoa atazitolea ufafanuzi Agosti 7, mwaka huu, na kesi hiyo itakapoendelea kutajwa na kuwataka washtakiwa kuendelea kukaa mahabusu.

Washtakiwa hao walipofikishwa mahakamani hapo Mei 6, mwaka huu na kusomewa mashtaka ya na Wakili wa Serikali Mkuu, Javelin Rugahuruza, akisaidiana na mawakili waandamizi wa serikali Shedrack Kimaro na Theophil Mutakyawa.

Hakimu huyo na wenzake walisomewa mashitaka 11 yalikiwamo ya kujihusisha na rushwa, kughushi na kujipatia mali kwa njia ya rushwa kati ya Juni Mosi, mwaka jana Aprili 15, mwaka huu, katika maeneo mbalimbali.

Mashtaka mengine ni kuchukua rushwa ya Sh. milioni 31.5 kutoka kwa Kangero, utakatishaji wa Sh. milioni 31.5 na kughushi nyaraka za uongo za nyara ya serikali za kilo 15 za meno ya tembo ya Sh. milioni 9.8.



Wadau wa madini ya Tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, wakiwa kwenye mkutano wa kujadili changamoto na mafanikio yao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanafunzi jamii ya wafugaji waanza masomo ufundi uashi

**Novatus Makunga,**
SIMANJIRO

WANAFUNZI 24 wa jamii ya wafugaji wa Kimasai wameanza rasmi masomo ya ufundi uashi katika awamu ya kwanza ya chuo pekee kinachotoa mafunzo ya ufundi stadi katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara.

Chuo hicho kilichoko katika Kata ya Emboret ambacho kimejengwa na shirika lisilo la kiserikali la ECLAT kwa kushirikiana na shirika la Upendo la Ujerumani, kimekabidhiwa kwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta).

Mratibu wa Veta Kanda ya Kati, Abdulkadir Yussuf, alisema juzi kuwa wameamua kuanza na mafunzo ya fani ya uashi, kutokana na mahitaji ya wananchi wa wilaya hiyo na wilaya ya jirani ya Kiteto ya mafundi wa ujenzi wa majengo.

"Kwa ujumla katika wilaya ya Simanjiro hivi sasa kuna kasi kubwa ya ujenzi wa nyumba lakini kuna changamoto kubwa ya mafundi wanatoka mjini Arusha kuja kujenga nyumba hapa," alisema.

Yussuf alisema katika awamu ya pili, chuo hicho kitaanzisha fani zingine zikiwamo ufundi seremala, umeme na bomba, ushonaji wa nguo na ufundi wa zana na mitambo ya kilimo.

Alisema chuo hicho ambacho mpaka kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 250, pia kitaanzisha mafunzo ya ufugaji wa kisasa na wa kibiashara wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku pamoja na wanyamakazi kama vile punda.

Pia alisema katika mwaka huu wa fedha, wameshatenga Sh. milioni 81 kwa ajili ya kujenga bweni lingine litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 24 katika eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 100.

Mwenyekiti wa ECLAT, Peter Toima, alisema wametumia Sh. milioni 531 katika awamu hiyo ya kwanza inayohusisha madarasa, bweni moja, jiko, vyoo, kisima kirefu cha maji, umeme wa nishati ya jua na vifaa vya kufundishia uashi.

"Tuliamua kujikita katika ujenzi wa chuo hiki kwa lengo la kuunga mkono mpango wa serikali wa kujenga vyuo vya ufundi stadi kwa kila wilaya huku tukizingatia kipaumbele cha wananchi wenyewe wa Simanjiro," alisema.

Naye Mwenyekiti wa shirika la Upendo la Ujerumani, Dk. Fred Heimbach, aliwataka wanafunzi hao wa awali kusoma kwa bidii kwa kuwa wamepata fursa ambayo inawahakikishia ajira na baadaye kuendesha maisha yao.

Diwani wa Emboret, Christopher Kuya, pamoja na wazazi wa vijana walioanza mafunzo hayo, walisema chuo hicho kitakuwa mkombozi kwa vijana wengi walioko mitaani baada ya kuhitimu darasa la saba na kidato cha nne kutokana na kushindwa kuendelea

## Vituo 149 kuboresha daftari la mpigakura

**Na Mwandishi Wetu,**
SIMANJIRO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, imetenga vituo 149 kwa ajili ya kuboresha daftari la kudumu la wapigakura na taarifa zao ili kuwawezesha wananchi kushiriki vyema uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwakani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Yefred Myenzi, alisema jana kuwa kazi hiyo imeanza tangu Julai 31 na inatarajiwa kuhitimishwa Agosti 6, mwaka huu.

Aliwataka wakazi wote wa wilaya hiyo ambao wana sifa za kujiandikisha au kuboresha taarifa zao, kufika kwenye vituo hivyo na kupatiwa huduma hizo.

Alitaja miongoni mwa sifa za watakaoshiriki uandikishwaji huo ni raia wa Tanzania, mkazi anayeishi sehemu husika mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea na wale ambao Oktoba, mwakani watafikisha umri wa miaka 18.

"Wale waliopoteza vitambulisho vya kupiga kura wanaweza kufika kwenye vituo hivyo na kupatiwa vitambulisho vipya na ambao hawakujiandikisha kipindi kilichopita, watapatiwa fursa hiyo," alisema Myenzi.

Alisema pia wataandaa taarifa za waliokosa sifa za kupiga kura ikiwamo walioopoteza maisha, waliohukumiwa vifungo magerezani na ambao wamebainika si raia wa Tanzania.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, aliwataka wakazi wote wa eneo hilo ambao wana sifa kuhakikisha wanatumia fursa hiyo kwa kujitokeza kwa wingi ili wajiandikishe au kubadili taarifa zao.

"Kuna baadhi ya watu walijiandikisha vitongoji vya Kairo au kijiji cha Naisinyai, huu ni wakati wao wa kubadili vituo kwa kujaza sehemu wanazoishi ili waweze kupiga kura kwenye uchaguzi mkuu wa mwakani," alisema Kobelo.

Mmoja wakazi hao, Happy Kayumbo alisema walemavu na wanawake wajawazito au wenye watoto wadogo wanapaswa kupewa kipaumbele wakati wa uandikishwaji huo.

## Walimu wapigwa 'stop' kubeba viboko darasani

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WALIMU wa madarasa ya awali hadi la tatu kote nchini, wamepigwa marufuku kuingia darasani na viboko kwa kuwa kufanya hivyo ni kuongeza woga kwa wanafunzi na kusababisha kushamiri kwa utoro.

Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Msingi kutoka Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), George Jidamva, alisema hayo jana akiwa kwenye ziara ya siku moja mkoani Kilimanjaro.

Katika ziara hiyo, Jidamva alitembelea shule za msingi za Kifumbu na Rau kuona juhudi za uboreshaji wa madarasa ya awali kabla ya kusambazwa nchini kote.

Alisema licha ya sheria kuruhusu wanafunzi kuchapwa voboko, utafiti unaonyesha kuwa mwalimu anapoingia darasani na kiboko, humtia mwanafunzi uoga na kusababishia wanafunzi wengi wa madarasa ya awali hadi la tatu kuchukia shule na kuacha.

"Watoto hao ni wadogo na wana uwezo wa kuonyeka bila kutumia fimbo. Naagiza walimu wote kuacha kutumia fimbo wanapoingia madarasani na badala yake kuwatengenezea wanafunzi mazingira rafiki ili kuwawezesha kuipenda elimu na kufanya vizuri katika masomo yao," alisema.

Alisema mbali na kutoingia na viboko madarasani, pia walimu wakuu katika shule za msingi kuhakikisha madarasa ya awali hadi la saba yanaongea vyema ili kuleta mabadilikio ya kimaarifa kwa wanafunzi nchini.

"Tumepata mradi katika mikoa ya Mwanza na Kilimanjaro, ambapo ulituwezesha kuwasaidia wanafunzi wa madarasa ya awali lakini mradi huo kwa sasa umeondoka na katika ziara yangu ya siku moja mkoani Kilimanjaro naona walimu wameweza kuuendeleza licha ya mradi huo kumaliza muda wake" alisema.

"Madrasa ya awali yanaongea, sasa nataka maofisa elimu mkoa wa Mwanza na Kilimanjaro hakikisheni mnakuwa walimu kwa mikoa mingine ambayo haikupata mradi huu ili kuhakikisha Tanzania nzima madarasa ya awali hadi la tatu yanaongea kupitia rasilimali zinazotuzunguka."

Aidha, aliwataka maofisa elimu ngazi ya kata kuwa wasimamizi wakuu wa kuhakikisha walimu hawaingii darasani na kiboko pamoja na kuhakikisha madarasa hayo yanaongea kwa rasilimali zinazopatikana katika mazingira yanayowazunguka.



Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Msingi, Ofisi ya Rais (Tamisemi), George Jidamva, akiwa kwenye darasa la awali, katika shule ya Msingi Rau, mkoani Kilimanjaro jana, ambapo aliwashughudia wanafunzi wakipata mafunzo kwa vitendo kupitia rasilimali zinazowazunguka. **PICHA: MARY MOSHA**

## NGO zaonywa kuhusu muda usajili

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MASHIRIKA yasiyo ya kiserikali (NGO) kwa Kanda ya Kaskazini yamehimizwa kujitokeza kwa wingi ili kujisajili upya na kwamba hakuna muda utakaoongezwa baada ya kumalizika ule uliopangwa.

Wito huo umetolewa kwa mashirika hayo ambayo awali yalisajiliwa chini ya sheria zingine lakini yanafanya kazi za kijamii, hivyo kutakiwa kusajili kwa Sheria ya NGO kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Namba 3 ya mwaka 2019.

Msemaji wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Vijana, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Erasto Ching'oro, alisema jana kuwa usajili huo unafanyika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro kuanzia Julai 29 na utafikia ukomo Agosti 6, mwaka huu.

Alisema NGO zote zinazofanya kazi za kijamii ambazo awali usajili wake ulifanyika katika mamlaka zingine kama Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita), Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wakala wa Usajili wa Leseni na Majina ya Biashara (Brela), usajili wake utakuwa umefutwa kama zitashindwa kujisajili chini ya Sheria ya NGO.

"Sheria inayataka mashirika hayo kujisajili chini ya Sheria ya NGO kwa kipindi cha miezi miwili, hivyo huu ni wakati wa mashirika kujitathimini yako wapi ili kufanya uamuzi sahihi kabla ya kipindi kilichotolewa na sheria hii kupita," alisema.

Aidha, Ching'oro alisema usajili huu unafanyika kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini yenye mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara na kutoa wito kwa mashirika yaliyopo katika mikoa hiyo kufanya usajili huo.

Alisisitiza kuwa usajili huo unafanyika bila malipo kwa mashirika yanayohusisha usajili lakini yale yanayojisajili kwa mara ya kwanza yanatoa malipo kwa ajili ya huduma hiyo.

Msajili Msaidizi Mkoa wa Kilimanjaro, Hilda Lauwo, aliyataka mashirika hayo mkoani hapa kuhakikisha yanashiriki usajili huo ili kuepuka usumbufu ambao unaweza kujitokeza baada ya muda uliopangwa kumalizika.

Naye mwakilishi wa Rita, Joseph Mwakatobe, alisema wako mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kutoa elimu na kufanya usajili wa mashirika mbalimbali ili kuleta tija kwa jamii na kugawanya rasilimali hizo nchi nzima.

Mmoja wa wawakilishi wa mashirika waliofika kupata huduma hiyo kutoka Gs Community, George Mayalla, ambao wanashiriki katika haki za binadamu kwa watoto na wanawake, alipongeza huduma hiyo na kuiomba serikali kuongeza muda wa usajili na kutoa elimu zaidi ili kuhakikisha elimu inafikiwa na watu wengi.

## Madiwani wagomea nyongeza ya kodi

**Na Mwandishi Wetu ,** MOSHI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Moshi limeazimia ukodishaji wa vibanda vya jengo la stendi kuu kwa wafanyabiashara waendelee kulipa gharama ya pango wanayolipa hivi sasa hadi muda wa mikataba yao itakapoisha Desemba, mwaka huu.

Katika mapendekezo yao waliyoyatoka katika kikao chao na Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Michaeli Mwendezi, kutokana na agizo la Waziri Mkuu alipokuwa mkoani hapa na baada ya mkataba kwisha, madiwani hao wamesema mapendekezo ya gharama waliyoyatoa yafikiriwe kama bei elekezi wakati wa kutangaza upya vibanda hivyo kwa kuzingatia taratibu za ununuzi.

Katika kikao cha baraza hilo kilichofanyika juzi, Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya, alisema hakuna namna wanavyoweza kubadili bajeti ambayo imekishwapitishwa bungeni wakati mwaka mpya wa fedha umeanza.

Alisema wapo kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii, hivyo wataendelea kuwahudumia kukidhi matakwa ya wananchi na wao ndio wawakilishi wao na kwamba watakapobadili bajeti, itasumbua mipango yote ya manispaa kifedha.

'Bajeti imepita lililobaki ni kuitekeleza hadi mikataba yao itakapokwisha Desemba, mwaka huu, hivyo waendelee kulipa pango kwa bei iliyopo hadi mwaka mwingine wa fedha. Baada ya hapo mapendekezo yao yatafikiriwa kwa mujibu wa hali ya soko itakavyokuwa," alisema.

Kwa mujibu wa Meya huyo, mapendekezo yao yatafanyika katika bajeti mpya na kuwa kuisumbua hii ya sasa ni kuyumbisha halmashauri, hivyo mikataba itakapokwisha mapendekezo yao yanaweza kuingia kwenye bajeti ya mwaka ujao.

Mbunge wa Moshi Mjini, Jaffary Michael, alisema tayari bajeti imepita wamiliki walikuwa wanalipa kati ya Sh. 400,000 na 600,000 na kwamba si madiwani waliopanga bali soko, hivyo ni vyema ikaachwa kama ilivyo hadi imalizikie.

"Mwezi Desemba tukitangaza tenda tutakabiliana na mabadiliko ya bajeti yetu. Hatuna vyanzo vingi vya mapato, maombi yao tutachukua na mapendekezo yao hatutayakataa. Tutafanyia kazi kutimiza matakwa ya wananchi wetu," alisema Michael.

Naye Diwani wa Njoro, Jomba Koi, alisema tatizo lililopo katika vibanda hivyo ni kuwa waliopangishiwa na manspaa nao wamepangisha kwa watu wengine, hivyo ni vyema kukafanyika umakini katika kuhakikisha anayepanga ndiye anakuwa mmiliki halali.

Kwa upande wake, Diwani wa Shirimatunda, Francis Shio, alisema ni vizuri wafanyabiashara nao waelewe kuwa wamiliki wa vibanda hivyo ni halmashauri na hawapangi bei kuwakomoa ila ni kutokana na watu walivyopendekeza na kuwa bei inabadilika kutokana na hali ya soko ilivyo.

Diwani Reward Shelukindo wa Kaloleni, alisema eneo hilo la stendi ni zuri kwa biashara ndiyo maana vibanda vyote vimejaa na ingekuwa bei inawashinda pasingekuwa na watu na hizo kelele wanazopiga ni kwa sababu ya mambo ya siasa tu.





Mkuu wa wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga (kulia), akiwasha moja ya pikipiki zilizokabidhiwa na Wizara ya Afya, Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa hisani ya Shirika la Umoja wa Mataifa la UN Women, kwa ajili ya maofisa maendeleo ya jamii wa Kata ya Chamwino, katika hafla fupi iliyofanyika ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Madiwani wafunguka kushuka kwa elimu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wamesema kushuka kwa elimu katika kata mbalimbali kunasababishwa na baadhi ya wazazi kutokuwa karibu na watoto wao.

Waliyasema hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha kufunga mwaka wa fedha 2018/19 na kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali. Diwani wa Kikuyu Kaskazini, Israel Mwansasu, alisema moja ya changamoto kubwa ya kushuka kwa elimu kwenye kata mbalimbali ni pamoja na wazazi kutokuwa karibu na watoto.

Alisema iko changamoto kubwa ya wazazi kutokuwa karibu na watoto wao katika usimamizi wa kufuatilia maendeleo ya elimu.

"Tumeona hapa baadhi ya kata zikifanya vizuri kielimu na wengine wakifanya vibaya, lakini haya yote yanatokana na wazazi kutokuwa makini na watoto wao.

"Wako baadhi ya wazazi ambao wamekuwa wakidhani kuwa kazi ya kumpatia elimu ni ya mwalimu pekee, wazazi hawana hata muda wa kuangalia madaftari ya watoto wao" alisema Mwansasu.

Naye Diwani wa Kikombo, Yona Kusaja, alitaka Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji na Idara ya Elimu watafakari ni kwa nini ziko kata ambazo zinafanya vizuri na zingine zinafanya vibaya.

Kusaja alisema liko tatizo la ikama ya walimu kati ya kata na kata na kuwapo kwa migogoro ambayo haitatuliwi kwa wakati.

Kutokana na hali hiyo, Kusaja aliitaka Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji na idara ya elimu kuhakikisha wanaondoa changamoto ambazo zinajitokeza kwa migogoro baina ya walimu au kukosekana kwa uiano wa ikama ya walimu kati ya kata na kata.

Akichangia sekta ya miundombinu, Diwani wa Zuzu, Awadhi Abdallah, alionyesha kuwa na hofu kuwa miradi isipotekelezwa ipasavyo, hawatapata kura katika uchaguzi mkuu ujao.

"Napenda kusema miradi hiyo ni mizuri na ipo kisheria na sisi madiwani hatuwezi kuipinga lakini kwa maana nyingine wasipofanya kazi yao vizuri kiukweli kupata kura itakuwa mbinde,"

# DC atangaza vita ukatili wa kijinsia

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

MKUU wa Wilaya ya Chamwino, Vumilia Nyamoga, amewataka maofisa maendeleo ya jamii ngazi ya kata kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyofanywa wilayani hapa.

Nyamoga alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akikabidhi pikipiki 12 kwa maofisa hao kwenye hafla iliyofanyika ofisini kwake.

Aliwataka maafisa hao kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo ufuatiliaji wa vitendo vya ukatili, uhamashishaji wa wananchi kujiunga na bima ya afya na kutoa elimu kwa vikundi ili kujiimarisha kiuchumi.

Kwa mujibu wa Nyamoga, Chamwino ni moja ya wilaya zenye idadi kubwa ya vitendo vya ukatili wa kijinsia mkoani hapa, hivyo ni imani yake kuona vitendea kazi hivyo vinatumika ipasavyo.

"Ninawaomba pikipiki hizi msitumie kuongeza nyumba ndogo kwa nyinyi vijana na nyinyi wasichana msitumie kuwatafuta vijana. Tumieni kwa malengo yaliyokusudiwa tafadhali," alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Asha Shame, alisema pikipiki hizo zimetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa hisani ya Shirika la Kimataifa la UN Women.

Alisema pikipiki zilizokabidhiwa zina thamani ya Sh. milioni 26.4 ambazo zitakuwa nyenzo muhimu kwa maofisa maendeleo ya jamii kwenye mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

"Tunatoa shukrani zetu kwa serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kutambua umuhimu wa kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Athumani Masasi, aliwataka maofisa hao kuhakikisha wanazitunza ili kuwafikia walengwa kwa wakati.

# Waandishi watwishwa zigo unyonyeshaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAANDISHI wa habari wametakiwa kutumia taaluma yao kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kunyonyesha watoto kutokana na hali ya unyonyeshaji kushuka.

Wito huo ulitolewa jana jijini hapa na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Lishe kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Moshi, alipokuwa akifungua semina ya waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani.

Alisema hali ya unyonyeshaji imeshuka na wanawake wengi hivi sasa hawanyonyeshi watoto ipasavyo na badala yake wanawapa vyakula vingine.

"Miezi sita ya mwanzo wanawapa vyakula vingine badala ya kuwanyonyesha maziwa ya mama pekee ambayo yana virutubisho vingi vya kumkinga mtoto na maradhi," alisema.

Naye Mratibu wa Lishe ya Mama na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sikitu Simon, alisema watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama miezi sita mfululizo wanapata madini chuma ya kutosha na kuwakinga na upungufu wa wekundu wa damu.

Alisema baada ya miezi sita mtoto huhitaji chakula cha nyongeza kutokana na kukua huku akisema ziko sababu zinazofanya mtoto kutopata maziwa ya kutosha.

"Sababu hizo ni pamoja na kuchelewa kuanza kunyonyesha, kupanga saa maalum ya kunyonyesha, kutonyonyesha usiku, kunyonyesha muda mfupi, kutomweka mtoto vizuri kwenye titi, kutumia chupa au vyombo bandia," alisema.

Alisema mtoto aliyenyonya vizuri titi la mama anakuwa na upendo huku akikemea tabia ya akina mama kuwanyonyesha watoto maziwa kwa kutumia chupa bandia.

Akizungumzia hali unyonyeshaji nchini, alisema watoto walioanzishwa maziwa ya mama baada ya kuzaliwa kwa mwaka 2018 ni asilimia 53 ikilinganishwa na mwaka 2015/16 ambapo ilikuwa asilimia 51.

Aidha alisema watoto walionyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji au vyakula kwa kipindi cha miezi sita kwa mwaka 2018 ni asilimia 58 huku mwaka 2015/16 ilikuwa asilimia 59.

Aliwataka akina mama kuacha uvivu wa kunyonyesha watoto ili kujiepusha na magonjwa ya mara kwa mara.



# Neema yanukia wakulima wa mwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema iko katika hatua za mwisho za makubaliano ya ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuchakata mwani kwenye eneo la Chamanangwe, Pemba.

Akifungua wa Maonyesho ya Nanenane jana Kizimbani, Mjini Magharibi Unguja, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Muhamed Shein, alisema ujenzi wa kiwanda hicho utafanyika kwa ushirikiano kati ya Zanzibar na kampuni ya Ocean Fresh na ile ya Kapa Carageenan Nusantara kutoka Indonesia.

Dk. Shein alisema kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda hicho kutasababisha mabadiliko makubwa ya kilimo cha mwani, uzalishaji wake, bei na maendeleo yake ya baadaye.

"Mwani ni zao linalozalishwa na kutegemewa na wananchi visiwani hapa, hasa kinamama. Kwa kuwaunga mkono wananchi hao katika jitihada zao za kulima na kuuza zao hilo, serikali imekusudia kuliendeleza zao hili," alisema.

Pia alisema azma hiyo ya serikali ni miongoni mwa ajenda zake kuu ambazo imezipangia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi izitekeleze kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda. Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko tayari kushirikiana na Indonesia katika kuhakikisha zao hilo linaimarika kwa kuwa Zanzibar ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa mwani duniani kwa sasa sasa.

Dk. Shein pia alisema azma mojawapo ya kufanya ziara ya kukitembelea kiwanda hicho ni kujifunza sambamba na kuangalia utaalamu unaofanyika kwa lengo la kupanua wigo kutoka kwa kampuni hiyo kubwa na yenye uzoefu wa muda mrefu nchini humo.

Kwa upande wake, uongozi wa kampuni ya mwani ya AGAR Swallow ya Indonesia, uliahidi kushirikiana na Zanzibar katika kukiimarisha kilimo cha mwani, zao ambalo limekuwa miongoni mwa mazao makuu ya biashara Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Hendrico Soewardjono, alisema azma yao ya kushirikiana na Zanzibar ni kuliendeleza na kuliimarisha zao la mwani.

Alisema kampuni hiyo tayari imepata mafanikio makubwa na bidhaa yake ya unga wa mwani ambayo hutengenezewa bidhaa mbalimbali za vyakula na dawa, imekuwa na soko kubwa na bidhaa zake huzisafirisha nchi mbalimbali duniani.

Alisema kuwa kutokana na Zanzibar kuliendeleza zao hilo na kulimwa kwa wingi, kampuni yake iko tayari kutoa ushirikiano unaohitajika ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo juu ya uendelezaji wa zao hilo na utafutaji wa masoko.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akipokea msaada wa vyerehani 94 vyenye thamani ya Sh. milioni 24 kutoka kwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Islamic Foundation, Arif Nahdi (wa pili kushoto), vilivyotolewa kwa ajili ya kuwagawia wananchi Visiwani Zanzibar ili kuweza kuzitumia katika kujiinua kiuchumi, katika hafla iliyofanyika visiwani humo jana. **PICHA: WMNN**

# Shule yabuni mradi kuongeza mapato

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHULE ya Msingi na Sekondari ya Kijini Mbuyu Tende, iliyoko Mkoa wa Kaskazini Unguja, imeanza uzalishaji wa mazao ya mboga na matunda kwa matumizi ya wanafunzi na kuongeza mapato kupitia mradi wa huduma za jamii wa 'Best of Zanzibar'.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Shule hiyo, Ulimwengu Mkadam Makame, alipokuwa akizungumzia kuhusu maendeleo ya mradi huo ambao umelenga kuongeza lishe kwa wanafunzi wanapokuwa katika masomo ya ziada.

Alisema mradi huo umeanza utekelezaji wake baada ya kupatiwa mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji kupitia Chuo cha Kilimo cha Kizimbani na kuratibiwa na mradi wa huduma za jamii.

"Mradi huu umelenga kuwapatia lishe wanafunzi na sehemu ya mapato yake kutumika kusaidia gharama za mahitaji ya shule. Tumeanza vizuri licha ya kujitokeza changamoto ikiwamo ya uharibifu wa mazao unaofanywa na mifugo," alisema.

Alitaja changamoto nyingine kuwa ni wizi wa miundombinu yakiwemo mabati ya uzio katika shamba na kuwataka wananchi kuwa sehemu ya walinzi pamoja na kuwaomba wafugaji kudhibiti mifugo ili kuepusha uharibifu wa mazao ulioanza kujitokeza.

"Wananchi lazima wafahamu mradi huu una manufaa makubwa kwa wanafunzi katika kuwapatia lishe wanapokuwa katika vipindi vya masomo ya ziada. Lakini pia utasaidia kupatikana fedha za mahitaji ya shule kama umeme," alisema.

Naye Ofisa Elimu wa Mradi wa Best of Zanzibar, Ali Suleiman Hamad, alisema wameamua kutoa mafunzo ya kilimo cha mboga na matunda ili kuibua chanzo cha mapato cha shule na kusaidia kuwapatia lishe wanafunzi.

Alisema mradi huo umekuwa ukitoa masomo ya ziada kwa wanafunzi wa sekondari katika masomo ya Kingereza, Hisabati na Sayansi kwa madhumuni ya kuinua kiwango cha ufaulu na wanafunzi kutumia muda wa ziada kubakia shule.

"Mradi huu ni sehemu ya chakula kwa wanafunzi, muhimu jamii kuunga mkono ikiwamo kushirikiana na uongozi wa shule kudhibiti vitendo vya wizi wa mazao na uharibifu unaofanywa na mifugo baada ya kuanza kujitokeza," alisema Hamad.

Alisema lengo kubwa la kuzalisha mboga na matunda ni kulitumia soko la mahitaji katika hoteli za kitalii na kuwataka wazazi kusaidia kufanikisha maendeleo ya mradi huo.

# Taasisi yamwaga vyarahani Kikwajuni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VYARAHANI 94 vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 vimetolewa na taasisi ya Islamic Foundation kwa wananchi wa jimbo la Kikwajuni ili kujiendeleza kimaisha kwa kufanya shughuli za ushonaji.

Akizungumza jana katika hafla ya kukabidhi vyarahani hivyo, Mbunge wa Kikwajuni, Hamad Yussuf Masauni, alisema msaada huo utasaidia kuwaongezea nguvu wajasiriamali katika kujiendeleza kupitia kazi zao

Masauni alisema katika kuhakikisha wananchi wanajitegemea katika ajira, ni vyema wajasiriamali wakajengewa mazingira bora ikiwamo kupatiwa nyenzo kama hizo kwa ajili ya kufanyia kazi zao.

"Katika taasisi za Kiislamu Tanzania ambazo zinaisadia jamii katika shughuli za kimaendeleo, taasisi hii inajitahidi katika kufanikisha hilo bila kujali dini ya mtu wala itikadi yake," alisema Masauni.

Alisema serikali itaendelea kuiunga mkono taasisi hiyo na taasisi zingine kuhakikisha zinaendelea kutekeleza majukumu yao vizuri ili wananchi wote hususani wale ambao ni masikini wafaidike.

Naye Mwenyekiti wa Islamic Foundation, Sheikh Arif Nadir, alisema lengo la kutoa vyarahani hivyo ni kuwasaidia wananchi kujikomboa kiuchumi.

"Lengo ni kuwawezesha vijana katika kujipatia kipato kupitia hivyo vyarahani. Tunawaomba wote ambao watapata nafasi ya kupata vyarahani hivi, wavitumie kwa lengo lililokusudiwa na si kwenda kinyume" alisema.

Naye Mwenyekiti ya Kituo cha Tayi, ambao ni miongoni mwa waliopatiwa vyarahani hiyo, Abdalla Omar, alisema ndoto ya kituo hicho ni kupata shule ya ushonaji lakini ndoto hiyo imekamilika baada ya kupata vyarahani na kuwataka wananchi wa Kikwajuni kutumia fursa hiyo kujifunza ushonaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



**NICKI MINAJ NAYE KUOLEWA**
Soma UK.20

JUMAMOSI AGOSTI 3, 2019



# FUMBO
# Nani mwenye ’Chuki’ na Aslay?

BASI SAWA



## Finally kumwita G Nako kwa 'Emergence'

MSANII anayechipukia katika muziki wa Bongo-flava, Abubakari Mrisho, maarufu kama Finally, anajiandaa kuachia kibao kipya ambacho amemshirikisha rapa G Nako.

Finally ametamba kuwa kuonekana kwa G-Nako katika wimbo huo unaoitwa 'Emergence' ni atua kubwa katika maendeleo ya muziki wake.

Msanii huyo kutoka lebo ya PMM amesema "Najisikia furaha kubwa kwani singo hii mpya itachochea mafanikio katika muziki wangu baada ya singo yangu ya kwanza 'Go down' kufanya vizuri."



## Nyoshi: Miaka 20 nimetoka patupu

MKONGWE wa muziki wa dansi, Nyoshi El Sadat, amesema katika miaka 20 ya kufanya kazi ya muziki katika bendi mbalimbali nchini hakupata mafanikio ya kujivunia.

Akizungumza hivi karibuni, Nyoshi amesema hakuna kitu ambacho anaweza kuonesha katika kazi hiyo, badala yake mali zote anazomiliki zinatokana na kazi yake binafasi.

"Kama Nyoshi anaweza kusema hakuna mafanikio katika kazi yangu ya muziki kwenye bendi nilizopitia, niliambulia patupu na hata magari na nyumba ninazomiliki nimepata kutokana na juhudi zangu binafsi na nguvu zangu," amesema Nyoshi.



# Mc Pilipili msimzogoe kabeba jiko kihalali

MCHEKESHAJI maarufu nchini, Mc Pilipili, amesema hakuna kifungu cha maneno kutoka kwenye kitabu cha Biblia ambacho amekosea wakati alipokula kiapo cha ndoa.

Mc Pilipili ametoa kauli hiyo baada ya kuwapo kwa mjadala mkali kuhusu maneno aliyotamka wakati akila kiapo cha ndoa yanayoonekana kwenda kinyume na mchungaji aliyesimamia ndoa yake.

"Hakuna nilichokosea wakati nakula kiapo kile, kwani katika biblia hakuna jambo hilo ila maneno yale yametungwa na sisi wenyewe hivyo hakuna sababu ya kusema nimekiuka kisheria na kuondoa uhalali wa ndoa yangu," amesema.

## INSTA-TWITTER





**Hanaga** makuu huyu mdada, kapole kenyewe. Nimeamua tu leo kumwambia nampenda. Nakupenda Yvonne. Usisubirie kuambiwa maneno matamu, anza kujiambia mwenyewe-**Monalisa.**



**Kama** wao vile kumbe sisi. Tupambaneni ndugu zangu ukweli utabainika Soon, Matunda mtayaona soon!!! ..Hakuna kukata tamaa nyinyi ni zaidi ya wale, tuwaachie wacheze Movie za kwenye makochi, sisi tudili na huku-**Mkude Simba.**




# Shilole atoa somo kwa wasomi

MSANII wa muziki wa Bongofava, Zuwena Mohamed 'Shilole', amesema ukarabati wa mgahawa wake umegharimu kiasi cha Sh. milioni 28.

Shilole amesema kujikita katika uuzaji wa chakula ni mfano wa kuigwa hata kwa wasomi wanaomaliza masomo yao kujiajiri.

"Wasomi wanaweza kutoboa na kutokuwa tegemezi kwa waliowasomesha kwa kujichanganya katika kuanzisha ubunifu wa kibiashara za kijasiriamali," alisema Shilole.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

## UNASEMAAA...

# Msondo, Sikinde zahamia nani zaidi Kanda ya Ziwa

BENDI kongwe za muziki wa dansi, Msondo Ngoma na Mlimani Park Orchestra zinatarajia kufanya maonesho katika mikoa ya Kanda ya Ziwa katika kile kichotafsiriwa kama Pambano la 'Nani zaidi'.

Katika pambano hilo ambalo ni la kwanza kufanyika nje ya jiji la Dar es Salaam litawapa fursa washabiki wa bendi hizo kuja na majibu ya ipi imeweza kukonga nyoyo za wadau wao.

Kwa mujibu ratiba ambayo kila upande umethibitisha ni kwamba, onesho la kwanza limepangwa kufanyika Agosti 8 maarufu kama 'Sikukuu ya Nane nane' mjini Kahama, katika ukumbi wa Chillers.

Meneja wa bendi ya Msondo Ngoma, Said Kiberiti, amesema onesho la pili la 'nani zaidi' limepangwa kufanyika mjini Geita siku ya Ijumaa ya Agosti 9 katika ukumbi wa Ambasador.

Alisema, onesho la tatu litafanyika Agosti 10 jijini Mwanza katika ukumbi wa Villa Park, ambapo tayari kuna mabishano makubwa baina ya washabiki wa bendi hizo mbili.



## BODA 2 BODA

# FUMBO
# Nani mwenye 'Chuki' na Aslay?



WIMBO mpya kutoka kwa mwanamuziki Aslay, unaobeba jina la 'Chuki' umezidi kuibua mambo mapya baada ya kudaiwa msanii huyo amewalenga baadhi ya watu wake wa karibu aliotoka nao Yamoto Bendi.

Hata hivyo, mwenyewe anaueleza kwamba wimbo guo unaotumia muda wa dakika 2 na sekunde 4, unatokana na visa vya kweli vinavyowapata mashabiki wake na hata mwenyewe kuchukiwa bila sababu.

Kuna watu wanamchukia mtu tu bila sababu, wao wanataka kuona anakosa maendeleo na kudidimia kila siku. Chuki hizi zipo kila mahali kwa sababu watu wa aina hiyo wapo na wataendelea kuwapo," anasema.

Baadhi ya watu walioshiriki katika mjadala mara kibao hicho kilipoachiwa, walikwenda mbali kwa kudai baadhi ya mistari inaweka wazi watu walioimbwa.

"Wimbo unaeleza wazi watu wanaomchukia hata kwenye mistari yake huna haja ya kufikiria zaidi kwani baadhi ya watu wake wa karibu kutoka kundi lake la zamani kwa sasa hawazungumzi nao," amesema Saidi wakati akishiriki video hiyo.

## INSTA-TWITTER


Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Ujana** huwa na maana mbili. Kuna ujana wa kibaiolojia. Huu unaupata tu hata ukiwa umelala umri unaongezeka na ujana huu huongozwa na vitu vya kimwili kama hasira, sifa , chuki wivu na kadhalika Pili kuna ujana wa maarifa. Huu ni lazima kuutafuta na kuupigania. Na huu unaongozwa na busara **-Dulla Makabila.**



**Kama** Samaki mkunje angali mbichi,basi mkubwa hakanyiki-**Rose Ndauka.**



**Usifanye** mchezo na madeni. Hii video inanikumbusha mbali. R.I.P mzee wangu King Majuto, inaniwia ugumu sana kurudi katika game tena-**Nisha Bebe.**

# Kuumbe!



WIZI MTUPU

## Mastaa Bongo Fleva funzo kwenu

KWA wanamuziki wa Bongo suala la kuiga nyimbo limekuwa jambo la kawaida. Mara nyingi utasikia wasanii wakubwa wanahusishwa na wizi wa nyimbo lakini hawachukuliwi hatua.

Baadhi ya mastaa wa Bongo fleva wamekuwa vinara wa kuiba nyimbo tena kutoka ndani au nje ya nchi, Kibaya zaidi wasanii hao wanawakwapulia hata wale wachanga bila kujali kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Lakini huko Marekani mambo ni tofauti, kwani ukijulikana umeiba mwimbo utakachokipata utaomba Mungu akunusuru.

Hivi karibuni mwimbaji maarufu Katy Perry amejikuta akitakiwa kuvunja benki yake baada ya kukutwa na hatia ya kuiba hatimiliki ya ngoma 'Dark Horse' ambayo ilidaiwa kuwa iliigwa.

Inaripotiwa kuwa Jumatatu ya July 29 mwaka huu Mahakama mjini New York imethibitisha kuwa wimbo huo wa 'Dark Horse' uliotoka rasmi mwaka 2013 ni hatimiliki kutoka kwenye wimbo wa 'Joyful Noise' ulioimbwa na mwimbaji wa Gospel Flame ambaye jina lake halisi ni Marcus Gray.

Imeelezwa kuwa prodyuza wa Katty Perry, Dr Luke alikiri mbele ya Mahakama kuwa hakuwahi kusikia wimbo wa Joyful uliotoka mwaka 2009.

Katty Perry alisema kuwa anaweza kuimba wimbo wake 'Live' mbele ya Mahakama lakini ilishindikana kutokana na wakili wake kupata hitilafu ya vifaa na kushindwa kucheza ngoma ya 'Dark Horse'.

Hata hivyo mmoja wa Wakili wa Flame alisema kuwa Perry aliwahi kuwa muimbaji wa Injili kabla ya kuingia kwenye ngoma za kawaida.

Imeripotiwa kuwa Mahakama imewakuta na hatia watu sita akiwemo muandaaji wa nyimbo na mtunzi wa nyimbo Sarah Hudson na Juicy J na kuelezwa kuwa itawekwa wazi kiasi atakachotakiwa kulipa Katy Perry kwa Marcus Gray.





## Majina yao tosha Bongo Fleva

**Na Adam Fungamwango**

KARIBUNI asilimia 70 mpaka 80 ya wasanii wengi wa muziki duniani hujulikana kwa majina kisanii na wala si yale yao halisi.

Wasanii wengi duniani hutumia majina ya kutungwa na mashabiki au kujipachika wao wenyewe, yakiwa na maana ya kile kitu wanachokifanya, au kifupi cha majina yao.


Lengo ni kufanya majina yao kutakika vizuri, tofauti na baadhi ya majina halisi ambayo mengine ni marefu ya hayaonekani kuwa na mvuto mbele ya wanaoyasikia.

Baadhi wanaamini kuwa kama wangetumia majina yao halisi basi wasingeweza kuwa mastaa kama walivyo hivi sasa.

Ndiyo maana kumekuwa na mlolongo wa wasanii wengi kuwa na majina yao maarufu ambayo si yao halisi, kiasi cha majina yao halisi yasijulikane kwa mashabiki.

Hata hivyo, wapo wasanii wachache ambao wao walivyoingia kwenye tasnia ya sanaa hawakutaka kubadilisha majina na pia waliona kuwa ustaa unatengenezwa na msanii mwenyewe pamoja na ngoma zake na wala si jina. Hawa ni baadhi ya wasanii wa bongo fleva maarufu nchini ambao wanatumia majina yao halisi, lakini bado wamekuwa na ushawishi kwa mashabiki kila kona.

### ASLAY ISIHAKA



Jina lake halisi ni Aslay Isihaka Nassor. Mwanzoni alijiita Dogo Aslay. Jina ambalo pia halikupindisha jina lake halisi. Na hata sasa ameendelea kujitambulisha kwa jina lake.

Mmoja wasanii vijana kabisa ambao wamekuwa mastaa akiwa wa umri mdogo.

### ALI KIBA

Ni msanii staa zaidi nchini Tanzania ambaye anatumia jina Lake Halisi. Ni nembo ya muziki wa bongo fleva Tanzania aliyeingia kwenye fani hii mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Kiba ameingia kwenye muziki wa bongo fleva kwa bahati tu, kwani ni mchezaji soka mzuri sana na ilikuwa asajiliwe na moja kati ya timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.


Hata hivyo pia alikuwa anajishughulisha na muziki wa kizazi kipya na tayari alikuwa amesharekodi ngoma ya 'Cinderella'. Wakati yuko kwenye harakati za kusubiria usajili, meneja wake alimfuata na kumwambia kuwa ngoma yake tayari imeshabamba nchini, hivyo aachane kwanza na soka, badala yake wakapige shoo Mwanza, baadaye akazunguka nchini nzima, hapo ndoto za kuwa mwanasoka maarufu nchini zikafa, badala yake akawa staa kwenye muziki wa kizazi kipya.

### VANESSA MDEE

Pamoja na kwamba jina lake la pili ni la kikabila, lakini hakujali hilo. Anajitambulisha kwa majina yake yote mawili. Na hata mashabiki wake wanamfahamu kwa majina yake yote. Ukimuuliza mtu msanii 'Vanessa'. Atakuuliza tena Vanessa Mdee?

Imedhihirika kuwa licha ya wasanii wengi duniani kuwa na majina yasiyo halisi. Lakini wasanii wa kike ndiyo wanaoongoza kwa majina ya kubuni. Lakini hili siyo kwa msanii huyu. Amekuwa mahiri pia kwenye muziki kiasi cha kujipatia umaarufu mkubwa.

### NANDY MFINANGA



Anaitwa Nandy. Yeye hujitaja kwa jina moja tu, tofauti na Vanessa Mdee. Ndiyo maana hakuna hata mmoja anayejua kama anaiwa Andy Mfinanga. Ni mmoja wa wasanii wa kike vijana ambao wamekuwa mastaa nchini wakiwa na umri mdogo. Umaarufu wake umetokana na kazi yake kubwa na ya kutoa ngoma kali zinazopendwa na mashabiki na wala si jina. Ni mmoja wasanii wachache ambao wanatumia jina lake halisi.

### MRISHO MPOTO

Ni mwimbaji, mtunzi na mashairi. Ana aina yake ya staili ya uimbaji wake ambao ni wa kughani mashairi. Amejipatia umaarufu mkubwa kutokana na aina yake hii muziki ambao maneno na ujumbe wake unafikirisha zaidi kuliko kukupa burudani ya kucheza.

Kutokana na aina yake ya muziki, muonekano, mavazi yake, na hata staili yake ya maisha, wala isingekuwa rahisi kwake kutumia jina la kubuni na kuachana na jina lake halisi.

Ni kwa sababu yeye mwenyewe ni muumini na utamaduni wa Mwafrika na maisha ya asili.

# Vijimambo




1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
22. Watu wa kizazi hiki, kweli wamedata. Haya bhana na selfii yako bandia - Mama Nah, Manzese DSM.
23. Kweli ushamba zigo la miba. Tangulini simu hiyo ikatumika kwa selifii? - Judi, Mbezi Mwisho DSM.
24. Hiyo ni sawa na kuosha mchele kwenye mto wa maji mengi. Utapata taabu sana - Semeni Mpanjira, Kilwa.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**






# Mpambe Nuksi: Tone la jasho halimwagiki bure

**Na Adam Fungamwango**

MTENDA mabaya siku zote hulipwa mabaya hapa hapa duniani. Pia jasho la mtu halipotei bure. Ujumbe huu umo ndani ya filamu moja kali iitwayo 'Mpambe Nuksi'.

Imechezwa na Ringo, Kipupwe, Mohamed Fungafunga maarufu kama mzee Jengua na wengineo.

Filamu inaanza kwa kumuonyesha mtu mmoja anayeonekana kuwa ana matatizo ya ugonjwa wa akili. Watoto wa mjini wanamwita 'chizi'. Hata hivyo chizi huyu ni wa ajabu kidogo. Ni tofauti na wengine tunaowafahamu.

Kibaka mmoja anampora dada mkoba wake pamoja na simu kichochoroni. Chizi huyo anashuhudia tukio hilo na kuamua kumkimbiza kibaka hadi akamkamata. Akavichukua vitu vyote na kumrudishia mwenyewe.

Siku nyingine dada mwingine anaangusha pesa alizokuwa anakwenda nazo sokoni kuchukulia mahitaji.

Chizi yule anaokota na kumrudishia mwenyewe. Kuna kijana mmoja anaitwa Mudi. Anadaiwa na Mpemba. Mpemba baada ya kuchoshwa na kudai anakuja na panga akitaka kumdhuru Mudi. Ni chizi huyo huyo akayelidaka panga na kumuokoa Mudi.

Tangu siku hiyo, Mudi akawa na urafiki na chizi huyo. Anatafuta muda na kwenda kumfuata jalalani ambako anakaa na kupiga naye stori, japo hawaelewani, lakini kitendo hicho kinawapa faraja wote wawili. Wale madada wawili waliofanyiwa wema na chizi hiyo Nasra na Shakila wanakutana. Kila mmoja anamsimulia mwezake ni jinsi gani alivyotendewa na chizi yule.

Kwa pamoja wanaamua kuungana na kuamua kumsaidia japo kwa kumpelekea chakula. Wanakwenda kule jalalani alikoweka makazi yake. Wanapata shida kidogo kwa sababu watoto wa mjini wanasema chizi ni chizi tu. Tabu walioipata wanasitisha kupeleka tena chakula.

Siku moja Shakila anapita eneo la jalala na kumkuta jirani yao Mudi akiwa amekaa na chizi huyo kana kwamba wanafahamiana kwa muda mrefu.

Akapeleka taarifa kwa shoga yake, na wote wakaamua kwenda kwa Mudi ili awaunganishie kwa chizi yule kwa sababu wametokea kumpenda kwa wema wake, lakini wanamuogopa.

Anawapeleka. Baada ya muda mrefu wa 'kucheza' naye jalalani, wote wanaamua kwa kauli moja kumchukua na kwenda naye nyumbani kumpa chakula, kumuogesha, kunyoa nywele na kumpa nguo mpya. Baada ya vyote kufanyika, nyumbani hapo kwa kina Nasra kuna kaka yake ambaye ni ustaadhi.

Yeye baada ya kumuangalia sana, aligundua kuwa ugonjwa wake wa akili haukutokana na Mwenyezi Mungu bali husda za watu. Anamuombea sana na hatimaye anarejewa na akili za kawaida. Hakuwa mwingine ila ni Ringo.

Anachokumbuka ni kwamba kabla hajawa hivyo alikuwa amemfukuza nyumbani mkewe mjamzito na kuleta mwanamke mwingine Hadija. Lakini pia alimkaribisha rafiki yake Kipupwe ambaye alifiwa na baba yake mzazi.

Ilibidi atoke na rafiki yake Mudi waende nyumbani kwake. Kufika huko akamkuta rafiki yake Kipupwe amekuwa kipofu.

Kipupwe aliposikia Ringo amerejea akaanza kulia na kuomba msamaha. Akatoa siri kuwa ni yeye ndiye aliyesababisha kuwa chizi. Alitaka awe mmiliki wa nyumba hiyo, hivyo akapanga mpango huo yeye na Hadija wa kumuendea kwa mganga wa kienyeji ili awe chizi.

Akasema kuwa yeye na Hadija ni wapenzi, lakini walifanya mpango mzima ili ajibebishe kwa Ringo, halafu amfukuze mkewe, Hadija aingia ndani ya nyumba, kabla ya kumfanya Ringo kuwa chizi na yeye Kipupwe kuimiliki rasmi nyumba akiwa na mpenzi wake huyo. Dili ilifanikiwa kwa miaka kadhaa, lakini sasa imebuma.



## JAY Z HAKUNAGA

# Aingiza nyimbo 100 Billboard

PENGINE Mungu yupo upande wao mwaka 2019 kufuatia wanandoa Jay Z na mkewe Beyonce kufanya kweli katika tasnia ya muziki.

Hivi karubini Beyonce aliishutua dunia baada ya kufyatua albam yake The Liones King: The gift' ambayo imekuwa gumzo kutokana na hatua yake ya kuwashirikisha wanamuziki kutoka Afrika.

Albam hiyo imeelezwa kufanya vizuri katika soko baada ya kununuliwa nakala zaidi ya 1,000,000 ndani ya masaa machache baada ya kuachiwa.

Wakati Beyonce akipaa kama mwewe katika mauzo, mumewe Jay Z ameripotiwa kuvunja rekodi baada ya kuingiza nyimbo 100 katika chati ya Billboard.

Kwa mujibu wa mtandao wa Hypebeast umeripoti kuwa Rapper Jay Z amevunja rekodi hiyo wiki hii baada ya kuingiza jumla ya ngoma 100 kama solo Artist kwenye chati hizo na kuwa msanii wa 6 kwenye historia.

Imeelezwa kuwa rekodi hiyo imekuja kupitia ngoma ya "Mood 4 Eva" aliyoshirikishwa na mkewe Beyonce na Childish Gambino ambayo ipo kwenye album ya 'The Lion King: The Gift'.

Wimbo huo umeshika nafasi ya 90 kwenye chart za Billboard Hot 100 na kuufanya kuwa wimbo wa 100 wa Rapa Jay Z kuwahi kuingia kwenye chati hizo.

Jay Z ambaye ameshika nafasi ya sita kwenye list hiyo anaungana na wakali kama The Glee (207), Rapper Drake (196), Rapper Lil Wayne (163), Elvis Presley (109) na Rapper Nicki Minaj (103)

# Nicki Minaj naye kuolewa



RAPA Nicki Minaj na mpenzi wake wa zamani wapo katika hatua ya mwisho ya kufunga ndoa.

Rapa huyo na mchumba wake Kenneth Petty imeelezwa wakati wowote wanaweza kutangaza harusi hiyo ambayo inaelezwa itakuwa ya kufa mtu.

Kulingana na TMZ kwamba Nicki na Kenneth wamesafiri pamoja kwenda Bev Hills Courthouse jumatatu ya wiki hii kwa lengo la kuchukua leseni ya kufunga ndoa.



## KimOprah ishukuru BBNaija kukutangaza

BAADA ya kutoka ndani ya jumba la Big Brother Nigeria yapata wiki tatu zilizopita, KimOprah, mshiriki huyo amepata umaarufu katika mitandao ya kijamiii.

Wakati KimOprah anajiunga katika shindano hilo likiwa katika msimu wake wanne, mrembo huyo alijulikana na wengi lakini hakuwa na mvuto kama alivyokuwa sasa.

Kupitia akaunti yake ya Istagram, alitupia picha mbalimbali za kuvutia na kusababisha idadi kubwa ya watu kuingia na kushirikisha picha hizo.

## We Willy Paul umeyataka mwenyewe

SERIKALI ya Kenya ipo njia panda kukubali wito wa wananchi wake wanaoshinikiza wimbo wa mwanamuziki Willy Paul, kufungiwa.

Wimbo huo mpya 'Lamba Nyonyo'. Umekuwa katika mgogoro mkali baada ya wanaharakati kijitokeza na kudai unawadhalilisha wanawake.

Baadhi ya wadau wamemuomba Mkurugenzi wa Bodi ya Filamu nchini humo, Dkt. Ezekiel Mutua kuufungia wimbo huo.





## Legend amchafua Donald Trump

HISIA kali zimetanda nchini Marekani baada ya mwanamuziki John Legend, kumuita rais wa nchi hiyo Donald Trump, kuwa ana tabia za kijinga.

Legend akiongea na TMZ Jumatano ya wiki hii amesemma "Nadhani Rais wetu anavijitabia vya kijinga, Mtu ambaye badala ya kutukutanisha yeye ndio kwanza anatugawa. Nadhani kuna ulazima wa kumtoa madarakani,".

Kwa wiki mbili sasa, Rais Trump amekuwa akishutumiwa kwa kutoa kauli za kibaguzi dhidi ya wabunge wanawake nchini Marekani pamoja na kuwaita panya wakazi wa jimbo moja nchini humo.

## Rick Ross, 50 Centi hawanogi

BIFU kati ya marapa wa Marekani, Rick Ross na 50 Cent linazidi kuwaka moto baada ya Rick Ross kukataa kufanya ngoma na msanii mwenzake kwa kudai ameshuka viwango.

Rick Ross akiongea katika mahojiano aliyoyafanya kwenye kipindi cha Big Boy Neighborhood na kusema kuwa kwa sasa yeye ni mfanyabiashara na anaona 50 Cent hana thamani kama zamani.

Mwanamuziki huyo ambaye ametoa Album yake ya kumi 'Port of Miami 2', alijibiwa haraka na 50 Cent a akisema kuwa hana mpango wa kufanya kazi na Rick Ross.



SAFU



Na John Juma
0716217615

## MIONZI YA SHERIA

# Mpangaji anaweza kupangisha?

SHERIA Namba Nne Sura ya 113 ya Sheria ndiyo inayotawala mustakabali wa upangaji na upangishaji. Mpangaji anajulikana, lakini swali ni kama baada ya kupangishwa yeye anaweza kupangisha.

Hata hivyo, kabla ya hilo tutazame vipengele muhimu vinavyotakiwa kuwa katika mkataba wa upangaji.

Ni muhimu kuangalia vipengele hivi kwasababu suala la uwezo wa mpangaji naye kupangisha ni moja kati ya migogoro kati ya wenye nyumba na wapangaji ambayo husababishwa na mikataba isiyoshiba kwa vipengele muhimu.

Kipengele kuhusu tarehe ya kuingia katika mkataba husika.

Kipengele kinachowatchambua wahusika katika mkataba mfano majina yote matatu, eneo analokaa au anwani kamili na nafasi zao zitajwe kuwa 'huyu ndiye mpangaji' na 'huyu ndiye mpangishaji.'

Kipengele kinachochambua vyema ardhi, kama ni nyumba, shamba mfano vyumba, stoo, jiko, ukubwa ekari na kadhalika. kama ni shamba.

Kipengele kuhusu kiasi cha kodi kinachotakiwa kulipwa namna ya ulipaji wake.

Kipengele kuhusu lengo la pango kama ni biashara, makazi na kama ni biashara ya aina gani;

Kipengele au vipengele kuhusu haki za mpangaji na mpangishaji katika matumizi ya ardhi husika;

Kipengele kuhusu sharti la kupangisha au kutokupangisha kwa mtu mwingine; Kipengele kuhusu nani anawajibika kufanya marekebisho;

Kipengele kuhusu notisi ya kuvunja mkataba na muda wake ielezwe katika mkataba.

Aidha, kuna kipengele kinachoambatana mwenye ardhi kuwa yote aliyomwambia mpangaji kuhusu hadhi na hali ya ardhi husika kuwa ni ya ukweli, mfano kuhusu mvua zikinyesha eneo halijai maji, nyumba haivuji na kila kitu kinamchotaka awe mkweli.

Kipengele kinachonyima au kutoa uhuru wa kuhuisha(renew) mkataba.

Jambo jingine lolote linaloweza kuwa muhimu sehemu ya sahihi na shahidi, Ni vyema shahidi awe wakili.

### MPANGAJI KUPANGISHA?

Ili mpangaji awe na uwezo wa kupangisha itategemea na aina ya mkataba alioingia na mwenye ardhi. Ikiwa mkataba umeweka bayana kwa kutoa uwezo kwa mpangaji kupangisha basi anaweza kufanya hivyo.

Lakini, ikiwa mkataba hautoi uwezo huo basi mpangaji hataweza kupangisha isipokuwa apate ridhaa kutoka kwa mwenye ardhi .


### KUBADILI MATUMIZI

Siyo tu mpangaji haruhusiwi kupangisha bali pia hata kubadili matumizi ya eneo au kufanya marekebisho bila taarifa na ridhaa kwa mwenye ardhi nalo litakuwa kinyume cha sheria ikiwa mkataba umekataza kufanya hivyo.

Zaidi ya hilo kifungu cha 93 cha Sheria ya Ardhi Sura ya 113, inakataza mwenye ardhi kucheléwa kutoa majibu ikiwa mpangaji kama ameomba ridhaa kati ya yaliyoelezwa.

### MASHARTI KUTOBADILIKA

Ikiwa mkataba utamruhusu mpangaji kupangisha basi hataweza kupangisha kwa masharti zaidi ya yale aliyo nayo yeye yaani aliyopewa na mwenye ardhi mwanzoni wakati akipanga. Pia muda wa kupangisha hautakuwa mkubwa kuliko ule uliopewa yeye na mwenye ardhi. Naomba kuwasilisha.



Na Reubeni Lumbagala

## KALAMU YA MWALIMU

# Kuchanganya masomo na mapenzi ni kutumbukiza mafanikio shimoni

WANAFUNZI wa kiume na kike, wanakabiliwa na changamoto ya kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi masomoni, hali inayohatarisha mustakabali wa safari ya masomo na maisha yao kwa ujumla.

Baadhi ya wanafunzi huanzisha uhusiano baina yao na wengine, hujiambatanisha na wasio wanafunzi. Katika picha ya ujumla wao, ni jambo la hatari iwe kati yao wenyewe na hata kuhusisha walio nje ya ulingo.

Mwanafunzi aliyeko shuleni, anapaswa kuzingatia siku zote kuwa, muda wa uanafunzi wake, jukumu lake ni kusoma kwa bidii ili afanikiwe kielimu na si vinginevyo.

Kujihusisha kimapenzi kwa mwanafunzi ni kufifisha ndoto zake mwenyewe, kwani mchanganyiko wa elimu na mapenzi, daima inaleta matokeo hasi kwa wahusika.

Masomo yanayofundishwa shuleni yanahitaji utulivu wa akili na umakini, ili kuweza kuyaelewa na kufaulu mitihani utakaowakabili. Hivyo basi, kichwa cha mwanafunzi hakihitaji michanganyo bali kupokea maarifa, ujuzi na stadi pekee kutoka kwa walimu ambao ndio wenye wajibu wa kufanya kazi hiyohivyo.

Wanafunzi wanapaswa kuzingatia sheria na kanuni za shule, ambazo zinapiga marufuku wanafunzi kujihusisha na mapenzi.

Kwa wanafunzi baina yao, muhimu ni kushirikiana kitaaluma, ili wafanikiwe. Mwanafunzi wa kiume amuone yule wa kike kama dada yake, vivyo hivyo mwanafunzi wa kike amuone wa kiume kama kaka yake.

Dhana hii ikiumbika kwa wanafunzi, itatokomeza changamoto ya wanafunzi kuanzisha uhusiano wa kimapenzi inayochangia kutokea mimba zisizotarajiwa, wanafunzi kufukuzwa shuleni na hata kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Wanafunzi pia, wajiepushe kuanzisha mahusiano ya kimapenzi na watu walio nje ya na mfumo wa elimu. Pamoja na kwamba wanafunzi mabinti wanakabiliwa na vishawishi vingi kuliko wenzao wavulana.

Lakini bado ni msimamo wanafunzi wa kike wana wajibu wa kuwa na misimamo thabiti usiyoyumbishwa katika kukabiliana na vishawishi hivyo, hatimaye kumaliza salama masomo na kamwe wasiishie njiani.

Wapo wanaume wanaotumia fedha na hadhi zao kutaka kuwarubuni mabinti wanaosoma, kwa kuanzisha uhusiano wa kimapenzi.

Wanafunzi wa kike wanapaswa kutanguliza shauku ya kutaka kupata elimu kwanza, kuliko jambo jingine lolote litakalojitokeza mbele ya safari yao kielimu.

Inajulikana kuna wanaume wanaojaribu kutumia changamoto za kiuchumi za baadhi ya wanafunzi wa kike watokao katika kaya maskini, wakitaka kuwachezea maisha yao.

Katika majaribu hayo, baadhi ya wanaume huwarubuni wanafunzi wa kike kwa kuwapa lifti kwenye vyombo vyao vya usafiri kama pikipiki na magari, ili kuwanasa kirahisi na wengine hutumia fedha au kununua zawadi kama nguo na vyakula kuwateka wanafunzi hao wa kike.

Hivyo, mabinti wanapaswa kuthamini utu wao kuliko zawadi za muda zinazotolewa na wanaume 'mafataki' zitazowasababishia mimba, Ukimwi na hata kufukuzwa shule.

Wanafunzi wafahamu zilivyo hatari za magonjwa kama Ukimwi na mengine ya zinaa; kisonono na kaswende. Ushiriki wao katika kimapenzi ni kuharibu mwelekeo wa maisha yao.

Wanafunzi wakitanguliza kiu ya kutaka kupata taaluma kwanza na kuachana na mapenzi, hapo maendeleo yao ya kitaaluma yatakuwa mazuri, kwani wafahamu akili zao zitajikita katika taaluma pekee.

Wanafunzi wahakikishe wanatumia muda wao kusoma kwa bidii, kutafuta kuyaelewa vizuri yale wanayofundishwa na walimu darasani, hali itakayowafanikisha katika mitihani ya ngazi zote hadi Taifa.

Mwanafunzi asidanganyike kuwa ana uwezo wa kufanya mawili (elimu na mapenzi) kwa wakati mmoja. Kamwe haiwezekani na daima "mshika mawili, moja humponyoka."

Kwa kuchanganya mapenzi na masomo, mwanafunzi anaingia moja kwa moja katika hatari ya kushuka kitaaluma na hata kufukuzwa shule.

Wanafunzi wathamini gharama kubwa ambazo wazazi wanazitumia katika kuwapatia mahitaji ya muhimu ili kuwawezesha wasomi vizuri.

Kwa wananchi 'mafataki' wanaowarubuni wanafunzi, waache mara moja tabia mbaya kwani wanafunzi ni sawa na watoto au ndugu zao ambao nao wanataka kusoma, ili kutimiza malengo yao.

Pia, wafahamu kuwa serikali ipo kazini katika kuwashughulikia wote wanaowarubuni wanafunzi na kuwaharibia masomo yao.

Sheria iko wazi kwa atakayejihusisha ma uhusiano na mwanafunzi, adhabu yake ni miaka 30 jela. Kwa hiyo, kujihusisha kimapenzi na mwanafunzi ni kujiweka katika mazingira ya kutumikia kifungo hicho.

Serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 23 kila mwezi kugharamia 'Elimu Bila Malipo' ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora.

Yeyote anayewarubuni wanafunzi ni kikwazo cha utekelzaji wa sera hii, hivyo hatua za haraka zichukuliwe dhidi ya watu wa aina hiyo. Wanafunzi someni kwa bidii mtimize malengo yenu. Shule kwanza, mengine baadaye. Tafakari.

■ **Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, wilayani Kongwa, mkoa wa Dodoma. Simu yake: (+255) 764 666349**

MADHILA YA

# Mama alipoangukia mtihani wa

## ■ Tabasamu lililopitiliza ghafla liligeuka huzuni kuu

JOVAN' alikuwa akiishi kwa raha na mume wake na watoto wao watatu katika kijiji cha jamii ya Yazidi nchini Iraq.

Wanamgambo wa Islamic State (IS) walipovamia kijiji hicho alitekwa na kupelekwa katika soko la watumwa ambapo aliuzwa kwa mpiganaji wa kundi hilo na kuzaa nae.

Wote wawili waliponea chupuchupu mashambulizi ya wanamgambo lakini alilazimika kuchagua kati ya familia yake ya Yazidi na mtoto wake mchanga aliyeitwa Adam.

"Nilimpenda mwanangu mara nilipomsikia akilia kwa mara ya kwanza...alikuwa mwanga gizani," anasema Jovan.

Hata hivyo, cha kusikitisha kwa upande mwingine ni kwamba baba yake Adam alikuwa mtekaji katika kundi la IS.

Kabla ya kadhia hii, Jovan alifurahia sana maisha, aliishi na mume wake Khedr na watoto wao watatu katika kijiji kizuri walichokulia tangu utotoni.

"Nilikuwa na raha na maisha yalikuwa mazuri kadri ya uwezo wangu," anasema.

Jovan anabainisha kwamba maisha hayo yalibadilika kabisa msimu wa kiangazi wa mwaka 2014.

"Siku moja mwanzoni mwa mwezi Agosti, muda mfupi baada ya kula chakula cha mchana, gari mbili zilizokuwa zimefungwa bendera nyeusi ziliwasili katika kijiji chetu,"anasema.

Jovan na Khedr hawakuwa na uhakika ya kilichokuwa kikifanyika lakini walifahamu fika wapo hatarini.

Ni wazi kwamba wanaume hao walikuwa wapiganaji hatari wa kundi la Islamic State (IS).

Hata hivyo nyuso za baadhi ya wapiganaji hao zilitambulika na ikabainika kwamba wanatoka kijiji cha jirani.

Aidha mumewe Khedr aliwafahamu. wanaume hao ambao waliwaahidi kuwa hawatawadhuru, bora washirikiane nao.

Familia yao na zingine 20 zililazimishwa kujiunga na msafara kutoka kijiji kimoja hadi kingine katika bonde la Sinjar.

Kile ambacho hawakukijua ni kwamba IS walikuwa na mpango wa kuwashambulia kutoka pande zote za mpaka wa Iraq na Syria.

Mwanzoni mwa mwaka huo wa 2014, Kundi hilo liliteka miji iliyo karibu na jiji la Baghdad.

Mji wa Mosul, ambao ulikuwa karibu na kijiji cha Jovan na Khedr, pia ulitekwa miezi mitano baadaye IS wakiwa tayari wamekwishaanza tena ajenda yao.

Habari zilisambaa haraka katika vijiji vilivyopo karibu, na nusu saa baadaye, wanavijiji wengi walikuwa wametorokea nyanda za juu za mlima wa Sinjar.

Agosti mwaka huo, Umoja wa Mataifa (UN) ulieleza kuanza kwa madhira mabaya kwa wakazi wa Kaskazini mwa Iraq na mwanzo wa ukatili dhidi ya binadamu.

Kiongozi wa msafara alimwambia Khedr kwenda milimani kuwashawishi wanavijiji kurejea nyumbani na kwamba hawakuwa na mpango wa kuwadhuru.

"Tuliwasilisha ujumbe huo lakini hakuna mtu aliyeamini na mmoja wa waliotorokea milimani alikuwa ndugu yangu," anasema Khedr.

Khedr alitaka familia yake irejee nyumbani lakini ndugu yake alipinga wazo hilo kwa hofu ya hatari iliyokuwa ikiwakabili.

Wanamgambo wa IS wanafahamika kwa kuwachukua kwa nguvu wanaume na kuwatumia kuwaua watu kwa niaba yao.

Khedr, sawa na mkewe alikuwa na hofu hususan kuhusu jamii ya kidini ya Wayazidi.

Hawakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yoyote, wale waliotorokea mlima Sinjar walikwama huko bila maji wala chakula na mamia ya wengine walifariki kutokana na baridi kali.

Maelfu ya Wayazidi waliosalia chini ya mlima huo walitekwa na wanamgambo wa IS.

Familia zilitenganishwa na wavulana walilazimishwa kujiunga na kundi hilo la kigaidi na kupewa mafunzo katika kambi zao, huku wanawake na wasichana wakitumikishwa kama watumwa wa ngono.

Wanaume waliokataa kujiunga na dini ya Kiislam waliuawa. Hakuna mtu aliye na uhakika ni Wayazidi wangapi walitekwa nyara na wanamgambo wa IS.

UN inakadiria kuwa Wayazidi 400,000 walikuwa wakiishi mjini Sinjar wakati huo na kwamba maelfu ya watu waliuawa.

Na zaidi ya watu 6,400 walikuwa Wayazidi, wengi wao wanawake na watoto ambao walifanywa watumwa, baadhi walibakwa, kupigwa na kuuzwa.

Jovan na watoto wake watatu na takriban wanawake na watoto 50 katika kijiji hicho waliingizwa kwenye lori na kusafirishwa hadi mji wa Raqqa nchini Syria ambao ulikuwa makao makuu ya kundi la IS.

"Hatukuweza kufanya lolote kujilinda...hakuruhusiwa kumuona tena Khedr kwa miaka mingine minne," anasema Jovan.

**KUZUILIWA**

Jovan alibaini baadaye sehemu aliyopelekwa kwamba ilikuwa Soko la watumwa mjini Raqqa.

Yeye na watoto wake walizuiwa katika nyumba ya ghorofa tatu iliyojaa wanawake na watoto karibu 1,500.

Anasema aliwafahamu baadhi ya wanawake hao ambao walikuwa jamaa zake na wengine majirani kutoka vijiji tofauti.

"Tulijaribu kufarijiana kwa kupeana matumaini kwamba muujiza unaweza kufanyika tukaachiwa,"anasema.

Badala yake, Jovan alilazimishwa kuamua anataka kupekwa kwa kundi lipi la wanamgambo wa IS.

Alipewa mwanamume wa Kitunisia aliyepewa jina la utani la Abu Muhajir al Tunisi, kamanda wa ngazi ya juu ambaye alikuwa mdogo, mwembamba na mwenye madevu yaliyowekwa nadhifu.

Jovan alitarajiwa kujiunga na dini ya Kiislam na baadaye "kuolewa" naye.

Alilia kwa siku kadhaa. Alijaribu kutoroka mara tatu, lakini watoto wake walitibua mpango huo kwasababu walikuwa wadogo, Haitham mkubwa, alikuwa na miaka 13, lakini Azad, ambaye ndiye mdogo alikuwa na miaka mitatu.

Kila alipojaribu kutoroka Abu Muhajir aligundua njama yake na kumfungia katika chumba kimoja.

"Nilitamani kujitoa uhai lakini nilipofikiria mateso watakayopitia watoto wangu nilibadili nia...pia niliwaza kuwaacha nitoroke lakini nilishindwa kufanya hivyo kabisa," anasema.

Hatimaye Jovan hakuwa na chaguo zaidi ya kujiunga na dini ya Kiislamu na hatma yake kukomea hapo.

**ATHARI**

Jovan aliathiriwa vibaya kiakili na hapendi kusimulia aliyopitia mikononi mwa mtekaji wake ingawaje alimruhusu kusalia na watoto wake na kuahidi kuwatunza wote.

Watoto wengi wa Wayazidi walitenganishwa na mama zao, wavulana walipelekwa katika kambi ya mafunzo ya kijeshi na wasichana walifanywa watumwa wa ngono na wafanyakazi wa nyumbani.



Baadhi ya wanavijiji wakikimbilia milimani kujificha wasishambuliwe na wanamgambo wa IS.**PICHA: MTANDAO**

Jovan, watoto wake na mwanamume wa Kitunisia 'aliyemuoa'walihamia nyumba moja mjini Raqqa, ambako alifanikiwa kutoroka.

Kufikia wakati huo IS walikuwa wanadhibiti maeneo mengi nchini Iraq na Syria, eneo linalolingana kwa ukubwa na Uingereza, kwa mujibu wa kituo cha Kitaifa cha Marekani cha kukabiliana na Ugaidi.

Asipokuwa katika mapigano, Mtunisia huyo alitimiza ahadi yake ya kuwatunza vizuri Jovan na wanawe, kwa kuwapeleka kucheza katika bustani moja ndogo karibu na nyumbani.

Hata hivyo katika miezi mitano ya kwanza ya mahusiano yao, Jovan aligundua amepata ujauzito.

"Hapakuwa na dawa na sikujua la kufanya,"anasema.

**MASHAMBULIZI**

Vikosi vinavyoongozwa na Marekani vilikuwa vikishambulia kwa mabomu ya angani maeneo yanayokaliwa na wanamgambo wa IS karibu kila siku.

Wapiganaji wa Iraq na wale wa Kikurdi walifanya mashambulizi ya ardhini katika mipaka ya Syria na Iraq.

Mtekaji wa Jovan wakati mwingi alikuwa vitani hadi wakati mmoja akaamua kumuuza kwa mfuasi mwingine wa IS.

Mateka wa Yazidi walikuwa wakiuzwa mara kwa mara lakini alipogundua Jovan ni mjamzito alibadili mpango wa kumuuza.

Akiwa na ujauzito wa miezi saba, Jovan alipata habari kuwa Abu Muhajir ameuawa vitani.

Jukumu la kuwalea watoto sasa likasalia kuwa lake peke yake.

Adam alizaliwa wakati Raqqa ilikuwa ikishambuliwa karibu kila siku na vikosi vya muungano vinavyoongozwa na Marekani.

Hawa na Haitham walimsaidia mama yao kujifungua ndugu yao wa kiume. Jovan anasema watoto hawakuwa na uhakika wamchukulie vipi ndugu yao mdogo aliyekuwa na muonekano tofauti na wao.

"Nadhani watoto walimpenda, walimtunza vuzuri, hasa Hawa, ni binti yangu lakini pia ni rafiki yangu mkubwa... alimlisha Adam na kumbembeleza hadi alale."

Mashambulizi ya mara kwa mara yalimlazimisha Jovan na watoto wake kuhamia nyumba nyingine lakini maisha yalikuwa magumu sana kwao.

Chakula kilikuwa kidogo na wakati mwingine Jovan alilazimika kula kidogo na kuwaachia watoto.

"Wakati mwingine tulikula mkate na maji yaliyochanganywa na sukari kidogo...nilifahamu ya kuwa nisipokula sitakuwa na maziwa ya kumnyonyesha mtoto Adam, lakini sikuwa na jinsi," anasema.

Licha ya changamoto zote alizopitia anasema mtoto Adam

**MAKALA**

# MAHARAMIA

# chaguo mwanawe au mtekaji IS



alimpatia ujasiri wa kuendelea na maisha.

"Nilimpenda sana...nilifahamu baba yake hakuwa mume wangu halisi... baba yake alikuwa muuaji, lakini [Adam] alikuwa damu yangu," anasema.

**KUTOROKA**

Nyumbani Iraq, Khedr hakuwa na habari kumhusu mtoto huyo na wala hakuwa na ufahamu wowote ilipo familia yake.

Ilikuwa imeshapita miezi 14 tangu familia yake ilipotekwa, akimtafuta mke na watoto wake.

Kila aliposikia kuna mwanamke na watoto wameachiwa huru alikuwa akienda mpakani kuangalia kama ni familia yake.

Hatimaye alifahamu walipo kupitia mtandao wa walanguzi wa watu uliokuwa ukinunua wanawake wa jamii ya Wayazidi na watoto kutoka kwa wanamgambo wa IS. Khedr alihitaji kutafuta dola 6,000 kwa kila mtoto.

Haitham, Hawa na Azad waliunganishwa na baba yao. Hata hivyo Jovan alilazimika kusalia Raqqa kwa miaka mingine miwili. Hakuwa na uhakika iwapo Khedr angemkubali mtotoAdam.

Kwa miezi kadhaa Khedr alitafakari cha kufanya. Wafuasi wa imani ya Yazidi, moja ya dini ya iliyo na waumini chini ya Milioni moja kote duniani wanatakiwa kufuata sheria maalum ya kidini.

Moja ya kanuni ya sheria hiyo ni kwamba yeyote atakayejiondoa katika dini hiyo hawezi kurudi hadi uamuzi utolewe na baraza la kidini la Yazidi hasa kwa wanawake waliotekwa kwa nguvu na IS na kuingizwa kwa dini ya Kiislamu.

Lakini kwa watoto waliozaliwa na wapiganaji wa IS hali ilikuwa tofauti kabisa. Mtu anaweza tu kuzaliwa ndani ya dini hiyo wala hawezi kujiunga nayo. Mtoto anakubaliwa nyumbani ikiwa wazazi wote wawili ni Wayazidi.

Jovan sasa alikuwa akiishi na wajane wengine wa Kiyazidi waliokuwa wameolewa na watekaji wa IS.

Wanawake wote walikuwa wakiogopa kurudi nyumbani katika kijiji cha Sinjar kwa sababu wamevunja mwiko.

"Wengine wamezaa watoto zaidi ya mmoja na wapiganaji wa IS, sasa wanaogopa kujiunga tena na familia zao," alisema.

Hatimaye Khedr aliamua kuwa watoto wake wanamuhitaji mama yao, ndipo alipomwambia Jovan kuwa mtoto Adam anakaribishwa.

Jovan alisafiri kurudi kijijini kwao Sinjar na mwanawe Adam, miaka minne baadaye. Hata hivyo, siku chache baadaye hali ilibadilika. Anasema familia yake ilianza kumshawishi amtenge mtoto Adam.

"Walianza kunieleza umuhimu wa kufuata mafundisho ya kidini, na jinsi jamii haitawahi kumkubali mtoto wa Kiislamu ambaye baba yake ni mpiganaji wa IS," anasema.

Khedr alimpeleka Jovan kukutana na Sakineh Muhammed Ali Younes, msimamizi wa makazi ya watoto yatima mjini Mosul akitarajia kuwa atamshawishi mke wake kukubali kumuacha Adam hapo.

Sakineh anasema alitumia saa kadhaa akijaribu kumshawishi Jovan kukubali wazo hilo wakati huo anasema, Khedr alikuwa akilia kwa machungu, ambapo naye alikuwa akimwangalia mwanawe Adam, akisema hawezi kumtelekeza.

"Lakini imani ya jamii ya Wayazidi ni muhimu kuliko matakwa ya mtu binafsi. Mimi na mume wake tumekubaliana kuwa nitamchukua mtoto hata iweje. Na mwisho hatukuwa na budi kudanganya."

Sakineh alimwambia Jovan amuache Adam kwa wiki kadhaa, kwa sababu ni mgonjwa na anahitaji kupewa matibabu.


"Nilimwambia mtoto wako yuko chini ya uangalizi wangu hadi suluhisho kuhusu suala hili lipatikane."

**•Kwa mujibu wa taarifa za mtandao.**



Baadhi ya wapiganaji wa IS, katika operesheni zao nchini Syria mwaka 2014.**PICHA: MTANDAO**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 11 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Mtu anayeipenda nchi yake
6. Jina la zamani Myanmar
7. nchi ambayo ni bara
8. patia msaada
9. Taifa teule la Mungu
12.Mji mkuu wa Sudani Kusini 15.Mpango
17. nyanyasa 18.bali
19.Nyumba za Kimasai
21.Pelekwa kwa gari
24.Watu wote katika nchi
25.Daiana kwa watu waliokopeshana26. Pesa ya Aljeria
27.Misa kwa waumini

**Dondoo: Chini**

1. Baba au Mama
2. Mji wake mkuu ni Vienna
3. Pesa ya Marekani
4. Baghdad ni mji mkuu
5. Uchoraji, uchongaji, ususi
6.Balaa 9.Hutumika kufukizia
11.Tambiko 12. karibu ya:
13. Sehemu ya ardhi baina ya vilima viwili 14. Chombo cha bahaarini chenye silaha za kivita
15.Askari wa kukodiwa
16.Piganiwa 20. Tarakimu
22.Ndugu wa kike
23. Mno

## Jibu Na: 10

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | A | N | A | D | A | | S | | A | K | U | A |
| E | P | A | | H | | | H | A | M | A | | |
| N | A | I | R | A | | W | A | D | U | D | U | |
| Y | | R | I | N | D | I | M | A | | H | | S |
| A | M | O | S | I | | M | B | A | B | A | Z | I |
| T | | B | A | W | A | B | A | | | L | | S |
| T | | I | L | A | N | I | | M | J | I | N | I |
| A | | | A | | G | | | S | | K | | M |
| | | N | | D | O | N | D | O | R | A | | I |
| U | | G | | | L | | A | M | U | | | Z |
| M | W | A | N | Z | A | | K | I | P | A | J | I |
| B | | O | | | | | A | | I | | U | |
| A | | | K | I | B | A | R | U | A | | A | |

TANZANIA YA VIWANDA DODOMA...

# SIDO yawanoa wajasiriamali kuwa wazalishaji kimataifa bidhaa ngozi

## ■ Kambi ya bure imeibua ujuzi, vipaji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

UNAPOTAJA Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo nchini (SIDO), ni nyenzo ya kuhakikisha wajasiriamali wanapiga hatua kumiliki viwanda, katika safari yao kufikia uchumi wa kati.

Mkoani Dodoma, uwepo wa SIDO umewawezesha wajasiriamali wake kuwapa nafasi ya kutumia kituo kipya cha mafunzo ya utengenezaji bidhaa za ngozi, kwa ajili ya kutengeneza bidhaa zao, kilichoko eneo la Kizota.

Ni mafunzo yaliyojikita katika utengenezaji bidhaa za ngozi kwa wajasiriamali wanaume na wanawake, ambao baada ya mafunzo, wamekuwa wakitoa 'ofa' ya wahitimu kujitokeza kutengeneza bidhaa zao, ikiwamo kuziboresha kwa kutumia mashine za kituo hicho bure, chini ya uangalizi wa SIDO.

Katika orodha ya bidhaa zilizotengeneswa zimo viatu, mikanda ya kuvaa na ya kufungia wanyama, mifuko ya kuewekea simu, wakitumia mashine mpya, ambazo zimo katika hatua ya maboresho, kabla hazijaelekezwa sokoni.

Lengo la kuwapa 'ofa' hiyo wahitimu wa mafunzo katika kituo hicho, ni pamoja na kutaka bidhaa zao za awali watengeneze chini ya malezi ya SIDO, kwa azma ya kuwa ubora unaoleta ushindani katika masoko makubwa ya kitaifa na kimataifa.

Hiyo inafanyika kupitia mradi wa bidhaa za ngozi, unaosimamiwa na Meneja wa Kituo hicho na msimamizi wa mradi, Stephano Ndunguru, kwa kushirikiana na wataalamu, wakihakikisha wajasiriamali wa Dodoma 'wanatoka' kupitia biashara zao za ngozi.

Ni jambo linalowafanya wajasiriamali wa Dodoma na Nje ya jiji, kujitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zilizopo ndani ya kituo hicho, ikiwamo kuziboresha kwa kutumia mashine mpya za kituo zinazitumiwa kufundishia wajasirimali, ili kuongeza ujuzi katika utengenezaji bidhaa, iwe za vikundi au mtu binafsi.

Meneja Ndunguru anaiambia Nipashe kuwa, hicho ni kituo bora na kipo kwa ajili ya kuwainua wajasiriamali, kwa kutoa mafunzo ya utengenezaji bidhaa mbalimbali za ngozi wanazoziuza katika masoko tofauti nchini.

Ndunguru anaeleza umuhimu wa mafunzo tajwa kwa wajasiriamali, ni kwamba yanawaongezea ujuzi, ikiwamo kuwajengea uwezo wajasiriamali na kuwapa mbinu zaidi kujipambanua kutafuta masoko ya nje ya mipaka kupitia bidhaa wanazotengeneza.

"Nawaomba wajasiriamali msibweteke majumbani jitokezeni kupata mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi ili muweze kujiajiri wenyewe," anasema.

Ndunguru anasema, ujuzi walio nao, unapochanganywa na walichopatiwa na wataalamu wa SIDO, unawasaidia kuimarisha biashara zao, pamoja na kuwa na viwango bora vinavyowawezesha kuingia katika masoko mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Meneja huyo anasema ni mafanikio yatokanayo na malezi ya wataalamu wa SIDO kupitia kituo cha usimamizi wa bidhaa za ngozi, kilichoko Dodoma.

### MAPENDEKEZO

Ndunguru, anaziomba serikali za mtaa kuwatengea maeneo wajasirimali wa bidhaa za ngozi, ili jamii ijue eneo fulani zinapatikana bidhaa za aina hizo, ambazo ni muhimu kwenye sekta ya biashara, kwa sababu zina thamani kubwa sokoni.

Anasema kila mmoja akisaidia kwa kusimama katika nafasi yake na nchi ikielekea kwenye uchumi wa viwanda, basi sekta ya ngozi inabeba nafasi ya kuchangia kuongeza uchumi huo kwa kiasi kikubwa. Msukumo mkubwa unaanzia katika uhitaji kwa jamii uliopo wa bidhaa zilizotajwa, uko juu ndani ya nchi na nje.

Meneja Ndunguru anasema, kinachotakiwa sasa ni wajasiriamali na wadau husika kushirikiana kuhakikisha sekta inakuwa na ubora unaosaidia kuwashawishi wateja kujitokeza kununua na kutangaza bidhaa hizo.

"Naomba wajasiriamali wa Dodoma tumieni fursa hii kuchangamkia mafunzo yanayotolewa ili muongeze ujuzi mlionao," anasema Ndunguru.

### CHANGAMOTO

Ndunguru anasema moja ya changamoto zinazowakabili wajasiriamali, ni kukosa maeneo ya kufanyia biashara na ndio maana SIDO inasisitiza serikali za mitaa ziwasaidie kuwatengea maeneo yatakayokuwa maalumu kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa za ngozi pekee.

Anaeleza imani yake kwamba kikwazo hicho kikitatuliwa, itakuwa rahisi kwa wajasiriamali kufanikiwa kupitia bidhaa wanazotengeneza.

Ndunguru anawataka wajasiriamali wasibweteke, badala yake wajitokeze katika mafunzo yanayotolewa na SIDO, yatayowasaidia kufikia ubora wa bidhaa wanazotengeneza, kwa vikundi au mtu mmoja na matokeo yake ni kufanikisha ushindani uliopo sokoni.

Meneja anasema, idadi ya wanafunzi wajasiriamali inayojitokeza bado ni ndogo kwao, kwa sababu jiji la Dodoma hivi sasa limepanuka, jambo linaloongeza wigo wa biashara, wanapaswa kuchangamkia fursa inayotolewa na SIDO.

### WASHIRIKI MAFUNZO

Mshiriki wa mafunzo, Burhan Magandila, anasema kikundi cha sasa kushiriki mafunzo hayo umemsaidia kupanua wigo wa utengenezaji bidhaa za ngozi, ambazo zitamsaidia kuendesha maisha kutokana na kipato, ambacho atataingiza kupitia bidhaa hizo.

Magandila anasema, awali hakujua namna ya kutengeneza viatu vya ngozi vyenye ubora, lakini baada ya mafunzo amefaidika na hivi sasa anatengeneza bidhaa bora.

Anaeleza imani yake kwamba tija ya uzalishaji itokanayo na ushindani sokoni, ni matunda ya kuboreshwa kwa kiasi kikubwa mashine za kituo hicho, sasa anaishukuru SIDO kuwapatia fursa ya kuboresha bidhaa zao, jambo ambalo awali hawakulipata.

Mgandila anasema, baada ya mafunzo wamekuwa mstari wa kuwahimiza wajasiriamali wenzake wajitokeze kushiriki mafunzo mbalimbali yanayotolewa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

"Wana - Dodoma tusibweteke kukaa katika makundi vijiweni, badala yake tutumie muda wetu kushiriki mafunzo ambayo yanafaida," anasema Magandila. Mwingine ni Hagai Wille, kutoka wilayani Kongwa. Anayewataka wanawake wenzake wasibweteke majumbani, bali wautumie muda kujitokeza kwenye mafunzo yatakayowapa faida kubwa maishani.

Hagai anasema, binafsi amepata ujuzi anaoamini utamsaidia kuendesha maisha yake ya kila siku yeye na familia take.



Meneja wa Kituo cha Bidhaa za Ngozi (aliyesimama katikati), akiwasikiliza baadhi ya washiriki wa mafunzo. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU.**



Washiriki wa mafunzo wakiwa katika majaribio ya kutengeneza bidhaa za ngozi.

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 12

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

Na Adam Fungamwango




"Habari zako zote ziko hapa, leo ngoja nikupasulie. Unapokwenda huko disco kuna mwanamke huko nasikia unakuwa naye. Lakini safari hii ya mwisho mlipoenda alikuja na mabaunsa wanamlinda na kuwatafuta wale wanaocheza naye ili wawapige. Kwa bahati nzuri yule mwanamke hakuwataja, ndiyo ikawa pone pone yenu."

Maelezo hayo yalimshtuka mno Kadili. Mbali na kushangaa mama yake kujua kila kitu, lakini pia mshangao mwingine ni jinsi habari nzima ilimvimfikia kwa kupindishwa pindishwa.

Kuna kweli ndani yake, lakini si kwa jinsi mama yake alivyohadithiwa. Hakujua ni nani aliyekwenda kuongea umbea huo.

Walibadilisha eneo la mazungumzo kutoka dukani ambako walikuwa na wasiwasi napo kuwa siri zao zinavuja, lakini kule walikokwenda nako vile vile. Zimemfikia tena mama yake, tena zikaongezewa na chumvi juu.

"Sikiliza mwanangu, hao ni wanawake wa kupita. Hata ikiwa vipi huwezi kumpata msichana tajiri ukawa naye milele. Huwezi kumuoa. Unachoweza kufanikiwa ni kuwa naye tu kwa muda mfupi kwa sababu ya matamanio. Wewe ni masikini, huwezi kuwa na binti tajiri na mkadumu kwa muda mrefu. Kama ni kweli msahau kabisa na achana naye huyo binti, angalia masomo yako, baadaye utakuja kupata msichana mzuri utamuoa." Mama alitoa wosia.

Kichwani mwa Kadili ulikuwa ni wosia mzuri. Ni kweli hata yeye tayari alishaamua kuachana na mawazo hayo, ikiwa hata kwenda tena disco kule 'Blue Star'. Kwa sababu hata wakienda, tayari msichana huyo alisema hatokwenda tena hapo kwa sababu amebadilishiwa.

Aliwaza kuwa pamoja na yote hayo, mama yake ameshindwa kuelewa kuwa yeye na msichana huyo Edina walichoishia ni kucheza muziki tu na hakuna hata mmoja kati yao aliyewahi kuongelewa suala la mapenzi juu yao, japo ni kweli alitokea kumpenda.

"Mama nimekuelewa. Sitaki kusema zaidi. Lakini wewe ni mama yangu nafuata ushauri wako." Alijibu huku akiwa amejiinamia.

**Kichwani mwa Kadili ulikuwa ni wosia mzuri. Ni kweli hata yeye tayari alishaamua kuachana na mawazo hayo, ikiwa hata kwenda tena disco kule 'Blue Star'. Kwa sababu hata wakienda, tayari msichana huyo alisema hatokwenda tena hapo kwa sababu amebadilishiwa.**

******************************************

Ni mwezi mmoja sasa tangu tukio lile litokee pale kwenye ukumbi wa blue star. Tayari Kadili alikuwa ameshaanza kusahau kila kitu na kuendelea na maisha mengine.

Hata hivyo kilichoanza kumtisha ni meseji mbalimbali za vitisho alizokuwa akitumiwa na watu wasiojulikana.

Siku moja akiwa chumbani kwake iliingia meseji kwenye simu yake. Kwanza aliidharau kutokana na utitiri wa meseji za matangazo mara kwa mata kwenye simu yake. Lakini baadaye aliamua kuifungua.

"Kijana unajifanya mjanja kuchukua wanawake za watu ee. Sasa nakukanya, achana kabisa na Edina, vinginevyo kichwa chako halali yangu." Ilikuwa ni meseji kutokana kwenye namba mpya kwake.

Na hata alipojaribu kupiga ilikuwa haipatikani. Haikuwa moja. Kila baada ya siku mbili tatu alitumiwa meseji hizo. Lakini kwa sababu hakuna kilichotokea, akaaza kuzipuuzia na woga ukaisha. Hakumwambia mama yake, badala yake alimweleza rafiki yake mkubwa Meze.

Wote aliamua kukubaliana kuwa meseji zile zaidi ya 10 zilitoka kwa mtu mmoja ambaye anajaribi kumtisha Kadili kwa kudhani kuwa alikuwa na uhusiano na Edina.

******************************************

Gari aina ya Subaru ilisimama kando ya barabara ya Kwa Mtogole maeneo ya Tandale jijini Dar es Salaam.

Hakuna yoyote aliyewatilia shaka watu wawili wenye miili mkubwa waliotoka ndani ya gari hilo na kufuata kinjia kidogo kilichoelekea kwenye daraja la mto Ng'ombe.

Ilikuwa ni kama wanasoma ramani kule walikokuwa wanaelekea kwa sababu hawakuwa wenyeji.

Safari yao iliishia kwenye kijumba kimoja kidogo ambacho kilikuwa kimejengwa peke yake.

Kwa hali ya kawaida kijumba kile kilitakiwa kuwa banda la uani na si nyumba iliyojengwa peke yake.

Ilionekana kama ilijengwa vyumba viwili na sebule, lakini haikupigwa 'lipu', matofali yake yakiwa ni makuukuu, huku juu kukiwa na mabati yaliyobadilika rangi kutoka ya asili na kuwa meusi kwa sababu ya kukaa kwa muda mrefu na kuwa na kutu.

Juu ya mabati hayo kulikuwa na matairi makuukuu ya gari, pamoja na baadhi ya matofali ambayo yote kazi yake ilikuwa moja tu, kukandamiza au kuzuia mabati hayo yasing'oke kwa upepo, kwani misumari iliyopigiliwa mabati hayo, ilikuwa imechoka, na baadhi ilikuwa imeshang'oka.

Mabausa wale wawili walisimama nje ya nyumba hiyo walionekana kuongea, huku wakionekana kukubaliana kuwa walipokuwa wakipatafuta ni hapo.

Waliosogea kwa pamoja hadi kufika mlangoni. Ulikuwa ni mlango ambao nao haukueleweka ni rangi gani kutokana na rangi yake ya awali kuchujuka. Haukuwa na hadhi yoyote ya kuitwa mlango, zaidi ya kitu kilichowekwa hapo ili kuwahifadhi wanaoishi ndani wasionekane.

Kwa hali ya kawaida haukuwa na uwezo wa kumzuia hata kibaka kuupiga teke moja tu na kuingia ndani.

Mmoja aligonga mlango mara tatu. Ulifunguliwa nusu dakika baadaye. Aliyefungua ni kijana asiyezidi miaka 25. Alikuwa amevaa kaptura, pekupeku, mkononi akiwa na tonge la ugali. Kwanza alishangaa kuwaona aina ya wageni waliomtembelea. Si tu kwamba walikuwa ni wageni kwake, lakini pia walionekana ni watu mwenye miili mikubwa kwa sababu ya mazoezi, maarufu kama mabaunsa. Hakuwahi kuwa na rafiki wa aina ile.

Kwa mbali alihisi shari kwenye nyuso za wageni wake, lakini alijikaza, huku hofu ikianza kumuingia moyoni.

"Karibuni" Aliwakaribisha kwa sauti ambayo hata yeye mwenyewe alikuwa hana uhakika kama inatoka kwenye kinywa chake.

"Wewe ndiye Kadili?" Aliuliza baunsa mmoja ikiwa ni kama jibu ya ile karibu ya kijana yule ambayo haikujibiwa.

Kijana huyo alionyesha mshangao kiasi cha dakika moja, kana kwamba kuna kitu alikuwa akitaka kusema, lakini mwishowe akasema "Ndiye mimi."

"Unahitajika na Madame Pauline." Kuhitajika huko kulimshangaza sana Kadili. Hakuwahi kukutana na mtu wa aina hiyo.

"Ndiyo nani, mbona simjui?" Aliuliza.

"Sisi siyo jukumu letu kujua wewe unajua au humjui. Tumekuja kukuchukua wewe na kukupeleka kwa Madame Pauline ambaye ametutuma. Yeye anakufahamu kwa hivyo mtakwenda kutambua huko huko." Baunsa mwingine ambaye alikuwa hajaongea muda wote aliamua kuvunja ukimya.

Itaendelelea Jumamosi

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**KISIMA CHA BEI NAFUU: kilichokamilika tunakuchimbia** kisima na kukuwekea pampu,tutaacha maji yanatoka kisimani kwako tupigie 0714564651/0752737534.


**TUNASAFISHA VISIMA:** virefu na vifupi kwa kutumia machine za kisasa na tunapima ubora wa maji. gharama zetu nafuu,simu:0623528465/0655752175

**NJANI PROPERTY COMPANY (NPC):** tunauza na kununua nyumba,viwanja,mashamba,lete mali kwetu ununue/uuze kwa haraka simu:0714564651/0658910584.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



## VYETI VIMEPOTEA



115358002

**WISLEY N. ELISAMIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0129/0151** kilichotolewa na MARA SEKONDARI mwaka 2003. Cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.0322/0545** kilichotolewa na KOLILA SEKONDARI mwaka 2008. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi (Form IV): **DAR/GOG/RB/I/8125/2019.** Form VI: **DAR/GOG/I/8140/2019.**

## VYETI VIMEPOTEA



115358102

**DAUDI JUMA ISSANGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1685-0061** kilichotolewa na IKHANODA SEKONDARI mwaka 2011. Cheti cha Ualimu chenye **index namba E.0508-0119.** kilichotolewa na MPWAPWA CHUO CHA UALIMU mwaka 2014. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/3903/019.**

**RE:THE LAND ACT NO 4 OF 1999**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF REF:NO S.299108**
**REGISTERED OWNER: JOSEPH HALINDOGO**

**LAND:PLOT NO,"278" KILAKALA MOROGORO MUNICIPALITY**

**APPLICANT: ROMAN M.MKUDE**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu there of unless cause to the country is shown within thirty (30) days from the date of this publication.

The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** is found, should be derivered to the office of the ;Municipal Director, Morogoro Municipal Council,P.O BOX 166 Morogoro.

Issued by:

115358502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;148/2019**

**Ombi la ROSAMISTIKA CRISPIN MAHENDEKA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu CHAMKAGA CHANDE LUKUMBUZWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 02/08/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/07/2019

115358302

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**EDWIN DANIEL KITANGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 218 AWJ** Aina yake SALOON CAR. Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi, Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/182672/2019.**

115358402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**RESPICH ANTHONY KAZIMOTO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye namba za usajili **T202 DNH** rangi ya SIVER . Chassis namba **ACA210080960.**Engine namba **1AZ0254564** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/130865/2019**

115357902

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE & ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 56… OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late WILLIAM JAMES KANYAMALA of Dodoma, Dodoma region**

**And**

**In the matter of Application for letters of Administration by VICTORIA KANYAMALA AND JOSEPH ALEXANDER KANYAMALA of Dodoma, Dodoma Region**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and witness the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioners.

**Objections to the grant should be filed on or before 20th /08/2019.**
**Date 1st/08/2019**

115357802


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la Nipashe*

*kila siku Tupigie 0767 223 311*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SEMENYA KUTOTETEA TAJI LAKE




**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MWANARIADHA Caster Semenya anasema hatotetea taji lake la ubingwa wa dunia mbio za mita 800 Septemba mwaka huu, baada ya uamuzi dhidi ya kesi aliyowasilisha mahakamani kupinga, kuidhinisha viwango vya homoni ya testosterone miongoni mwa wanariadha wanawake.

Lakini mwanariadha huyo wa Afrika kusini amesema "ataendelea kupambana kutetea haki za binadamu" licha ya "kusikitishwa kwake".

Semenya amewahi mara mbili kukata rufaa dhidi ya sheria za IAAF zinazomzuia kukimbia bila kutumia dawa, lakini uamuzi unaomruhusu kukimbia sasa umebatilishwa.

Semenya anapinga sheria mpya za shirikisho hilo la riadha duniani IAAF zinazomtaka yeye na wanariadha wengine walio na utofuati wa ukuwaji kijinsia (DSD) lazima watumie dawa zinazopunguza homoni za testosterone ili kuweza kukimbia katika mbio za kuanzia mita 400 hadi maili moja au abadili mbio atakazoshiriki.

Semenya alikuwa anaweza kukimbia wakati akisubiri uamuzi wa mahakama ya Uswizi, na awali alishindwa katika rufaa aliyowasilisha katika mahakama inayoshughulikia mizozo katika michezo (Cas) mnamo Mei.

Katika ujumbe aliotuma kwenye mtandao wa Twitter, Semenya aliandika, "Nafsi inayojitahidi haiwezi kuzuilika."

Uamuzi huu wa sasa wa mahakama ya juu zaidi ya Uswizi una maana kuwa hatoruhusiwa kushindana katika mashindano ya ubingwa duniani huko Doha.

"Nimesikitishwa sana kuzuia kulitetea taji langu nililioshinda kwa ugumu," Semenya, mwenye umri wa miaka 28, amesema.

# Ronaldo ashtakiwa Korea Kusini

**SEOUL,** Korea Kusini

MASHABIKI wenye hasira wa Korea Kusini wanataka walipwe fidia baada ya Cristiano Ronaldo kushindwa kuingia uwanjani wakati wa mchezo wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya dhidi ya Juventus.

Nyota huyo wa Ureno alikuwa amesaini mkataba wa kucheza dakika 45 wakati mechi dhidi ya timu hiyo ya Ligi Kuu ya nyota wote ilipotangazwa, wanasema waandalizi, lakini alikaa kwenye benchi nje ya uwanja.

Mashabiki walijawa na ghadhabu wakati aliposhindwa kuonyesha ishara yoyote ya kuingia uwanjani, hata wakaanza kushangilia kwa kupaza sauti wakilitaja jina la Lionel Messi.

Baadhi ya mashabiki sasa wamekwenda hadi kwenye kampuni ya sheria mjini, inayofahamika kama Myungan kuwasilisha mashtaka.

Wanataka walipwe fidia ya won 70,000 (sawa Sh. 100,000 kwa tiketi) na fidia kwa kila mmoja kutokana na kile wanachokitaja kuwa "kuathirika kiakili ".

"Kwa kawaida katika hali kama hii mlalamikaji hulipwa gharama ya tiketi, lakini suala hili ninalichukulia kama swala la kipekee kwasababu kampuni , kupitia matangazo ya uongo, iliwalaghai mashabiki wa nyota huyo," alisema wakili kutoka kampuni ya mawakili katika mazungumzo na shirika la habari la Reuters.

"Kwa upande wa tatizo la kuathirika kiakili, ningependa kusema kwamba baadhi yao ni mashabiki sugu, mashabiki sugu kabisa. Kwa hiyo kwao ni uchungu mkubwa kwa sababu wanampenda Ronaldo na wanataka kumlinda, lakini hawawezi, kutokana na hali halisi ," aliongeza.

"Kwa sasa tuna walalamikaji ambao waliishtaki kampuni , lakini nimekuwa nikipokea simu nyingi leo na ninadhani ni zaidi ya simu 60,000 ."

Robin Chang, Mkurugenzi mkuu wa The Fasta, wakala wa Korea walioandaa mechi hiyo aliangua kilio mbele ya waandishi wa habari wa kampuni ya SBS na kuthibitisha kuwa mkataba ulieleza wazi kuwa Ronaldo angecheza kwa dakika 45.

Hata hivyo, Chang alibaini tu kwamba mchezaji huyo wa miaka 34 hatacheza mechi dakika 10 tu baada ya kipindi cha pili.







# *Alves asaini Sao Paulo*

**SAO PAULO,** Brazil

BEKI mkongwe wa Brazil, Dani Alves amesaini kuichezea klabu ya Sao Paulo FC akiwa mchezaji huru.

Klabu hiyo ilitangaza Alhamisi kuwa imemsajili beki huyo mwenye umri wa miaka 36 ambaye amewahi kuzichezea Barcelona, Juventus na Paris Saint-Germain.

Vyombo vya habari vya Brazil vimeripoti kwamba mkongwe huyo amesaini mkataba wa kuichezea timu hiyo hadi mwaka 2022 baada ya kombe la Dunia nchini Qatar. "Ningeweza kuchagua popote pa kucheza, lakini nilichagua kurudi nyumbani Brazil," alisema beki huyo wa kulia.

Mkataba wa Alves na PSG ulimalizika Julai na awali alisema kwamba angependa kubakia kucheza barani Ulaya. Beki huyo alikuwa nahodha wa Brazil kwenye michuano ya mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, ambao walilitwaa taji hilo.

## HABARI MICHEZO

# Tottenham yamsajili Giovani Lo Celso

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham imeripotiwa kukamilisha usajili wa kiungo wa Real Betis, Giovani Lo Celso kwa pauni milioni 55.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina atasaini mkataba wa miaka mitano wa kujiunga na Tottenham, kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo.

Lo Celso, ambaye alifunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho tano kwenye ligi Kuu ya Hispania, La Liga, msimu uliopita, alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua hapo Tottenham kipindi hiki cha majira ya joto.

Baada ya kuanza kucheza soka katika klabu ya Rosario Central, Lo Celso alijiunga na Paris Saint-Germain mwaka 2016, lakini akaishia kwenda kujiunga na Betis.

Tottenham ilimnunua Tanguy Ndombele kutoka Lyon kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 65 kipindi cha majira ya joto.

Kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino kitaanza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu Agosti 10 ugenini dhidi ya Aston Villa.






# BAYERN KUMFANYA SANE MCHEZAJI GHALI ZAIDI

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich itamfanya Leroy Sane kuwa mmoja wa wachezaji ghali zaidi wakati wote kama watamnunua winga huyo kutoka Manchester City.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, Man City wanataka kulipwa pauni milioni 135 ili kumuachia mchezaji huyo ambaye walimnunua kwa pauni milioni 37 miaka mitatu iliyopita.

Ada hiyo itakuwa sawa na ile waliyonunuliwa wachezaji kama Joao Felix, Philippe Coutinho na Ousmane Dembele kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita, huku Kylian Mbappe na Neymar pekee ndio gharama yao ilikuwa zaidi ya pauni milioni 150.

Guardiola ameonekana kukasirishwa na maofisa wa Bayern ambao wanaendelea kumshawishi Sane ili atue kwa miamba hao wa Bavaria.

Kocha, Niko Kovac hivi karibuni alizungumza hadharani kuwa anajiamini mchezaji huyo atatua pale kwenye dimba la Allianz Arena kipindi hiki cha majira ya joto.

City wamewaandikia mabingwa hao wa Bundesliga kuwataka kutomzunguzia hadharani mchezaji wao huyo, huku Kovac akimuomba radhi Guardiola kwa njia ya ujumbe wa simu.

Sane amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake na bado hajawa tayari kufanya mazungumzo ya kusaini mkataba mpya.

# *Pepe: Kama sio Arsenal ningetua Chelsea*

**LONDON,** England

NYOTA mpya wa Arsenal, Nicolas Pepe, amedai kwamba Chelsea ndio ilikuwa klabu pekee ya Ligi Kuu ya England ambayo angeweza kujiunga nayo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 alikamilisha usajili wa pauni milioni 72 kujiunga na washikabunduki hao wa London Alhamisi, akisaini mkataba wa miaka mitano.

Hata hivyo, katika mahojiano na Telefoot nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast alisema: "Chelsea, ndio ilikuwa klabu ya ndoto yangu. Ndio klabu pekee nchini England ningeweza kujiunga nayo."

Mshambuliaji huyo alikuwa mchezaji wa klabu ya Angers kabla ya kusajiliwa kwa ada ya pauni milioni 9 kujiunga na Lille Julai mwaka 2017.

Arsenal ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Angers Jumatano iliyopita, na ikashinda kwa penalti 4-3 baada ya kutoka sare ya kufungana bao 1-1.

Farid El-Melali alianza kufunga dakika ya 13 kabla ya Reiss Nelson kusawazisha dakika tano ya kipindi cha pili kwenye mchezo huo uliopigwa uwanja wa Jean-Bouin.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE AMSHAURI NEYMAR KUBAKI PSG

Afanya mazungumzo naye binafsi na kumwambia klabu bado inamhitaji...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe ameingilia kati kwenye mgogoro wa majaliwa ya Neymar na amebainisha kwamba amemshauri mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kubakia hapo PSG.

**Huku zikiwa zimebakia wiki chache kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili, Neymar amebainisha kuwa anamatumaini makubwa ya kurudi kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, na kutua katika timu yake ya zamani ya Barcelona.**

Mbappe sasa ameamua kuingilia kati na kuzungumzia sakata hilo kwa kubainisha kuwa amefanya mazungumzo binafsi yeye na Neymar na amemshauri kubakia klabuni hapo.

Gazeti la Catalunya la Mundo Deportivo limeripoti kuwa Mbappe amemshauri Neymar kutoondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto na kumtaka aendelee kucheza naye.

"Ni hali ambayo kila mmoja anajua, bado klabu inamhitaji na mimi nimezungumza naye kumshauri abakie hapa," alisema Mbappe.

"Namtaka yeye abakie na sisi. Anajua tayari kile ninachofikiria kuhusu hali hii, nimezungumza naye kiungwana na kwa heshima kabisa kumtaka abakie na sisi."

Neymar hivi karibuni alirudi kwenye kambi ya mazoezi ya PSG baada ya kupona, lakini bado ameweka msimamo wake wazi kwamba anataka kuondoka klabuni hapo."

Hata hivyo, kocha wake, Thomas Tuchel anaamini kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anaweza kubakia klabuni hapo.

"Nimemuona yuko fiti na anaonekana wazi kabisa yupo kawaida," alisema Tuchel wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hatima ya Neymar.

"Namuona yupo kawaida na anaonekana anaupenda zaidi mchezo wa soka, hivyo kuna nafasi ya yeye kuendelea kubakia hapa."

Kauli ya kocha huyo ameitoa siku moja baada ya Neymar kutamka hadharani kwamba hatavaa tena jezi ya PSG kucheza mechi yoyote msimu huu, kwani anataka kuondoka.

Neymar pia aligomea kufanya mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake ikiwa ni shinikizo la kutaka aondoke klabu hapo.

Nyota huyo wa zamani wa Santos alisajiliwa kwa dau lililoweka rekodi ya dunia wakati akitoka Barcelona na kutua hapo PSG miaka miwili iliyopita.

## ZISIKUPITE

### CITY YAMGOMEA SANE BAYERN

MANCHESTER City imekataa ofa ya pauni milioni 72 kutoka kwa Bayern Munich kwenda kwa mshambuliaji Mjerumani Leroy Sane, 23. ***(Metro)***

### DYBALA AIPASUA KICHWA UTD

MANCHESTER United inahaha kufikia makubaliano na mshambuliaji wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala na wawakilishi wake, kwa kuweka mpango wa kubadilishana na straika Mbelgiji Romelu Lukaku, 26. ***(Independent)***

### YAMSUBIRISHA MAGUIRE

BEKI wa England, Harry Maguire, 26, aliachwa katika kikosi cha Leicester City kilichocheza mechi ya kirafiki jana dhidi ya Atlanta kwa sababu ya sintofahamu inayoendelea kuhusu mustakabali wake wa baadaye, wakati huu 'Mbweha' hao wakihitaji pauni milioni 90 kama Manchester United inahitaji saini yake. ***(Telegraph)***

### ROMA YAMPANIA LOVREN

BEKI wa Liverpool, Dejan Lovren, 30, anawindwa na Roma na klabu hiyo ya Italia inaamini inaweza kumpata beki huyo wa kati raia wa Croatia kwa dau kati ya pauni milioni 11 na 12. ***(Gazzetta dello Sport, via Mirror)***

### CITY YATAJA DAU LA SANE

MANCHESTER City inataka pauni milioni 137 kwa Leroy Sane kama hatataka kusaini mkataba mpya, baada ya huu wa awali ambao unamalizika Juni 2021. ***(Telegraph)***

### LIVER YATUA KWA KAMANO

LIVERPOOL inataka kumsajili mshambuliaji wa Bordeaux na Guinea, Francois Kamano, 23, na ipo tayari kulipa pauni milioni 20. ***(Sun)***

### SPURS YAJITOSA KWA LO CELSO

TOTTENHAM inakaribia kukamilisha dili la pauni milioni 55 kwa kiungo wa Real Betis, Giovani lo Celso, 23, na mchezaji huyo anajiadaa kukubali kuangua wino mkataba wa miaka mitano. ***(Mundo Deportivo, via Mail)***

### UTD YAIACHIA EVERTON KEAN

MANCHESTER United imekataa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Moise Kean, na kutoa fursa kwa Mtaliano huyo kujiunga na Everton. ***(90min)***

### CAHILL AWANIWA PALACE

CRYSTAL Palace imejiunga katika mbio moja na West Ham United katika kujaribu kuipata saini ya beki wa kati wa England, Gary Cahill, ambaye ni mchezaji huru baada ta kuondoka Chelsea. ***(Mail)***

### AMCHELEWESHA SESSEGNON

TOTTENHAM inaamini itainasa saini ya beki wa kushoto wa Fulham na England U-21, Ryan Sessegnon - lakini ingependa kumtoa kwanza beki Danny Rose, 29. ***(Express)***

### OTAMENDI ANG'ANG'ANA CITY

BEKI wa kati wa Argentina, Nicolas Otamendi, 31, anataka kubaki Manchester City licha ya kuhusishwa na kuondoka klabuni hapo. ***(Sun)***

## ZFF yatoa darasa viongozi wa klabu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

Viongozi wa klabu wametakiwa kuisoma na kuielewa Katiba ya Shirikisho la Soka Zanzibar ikiwa ni pamoja na kanuni za mashindano ili waweze kuziongoza vema klabu zao kwa mujibu wa sheria za soka na shirikisho hilo kwa ujumla.

Hayo yameelezwa na Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, wakati akifungua mafunzo ya siku moja ya uongozi kwa viongozi wa klabu 20 za madaraja mbalimbali zilizopo katika Jimbo la Kwahani kisiwani hapa.

Kombo alisema ili kuzipata klabu zenye wachezaji wenye nidhamu ni vema viongozi hao kwanza wakawa mfano mzuri kwa kufuata misingi ya Katiba ya ZFF na hata kanuni za kuendesha mashindano ya shirikisho hilo ili kujiepusha na vitendo vichafu vinavyofanywa na baadhi ya viongozi ikiwamo kupiga waamuzi huku wakijua kufanya hivyo ni kosa.

Alisema mafunzo hayo ya uongozi yamekuja muda muafaka ambapo wanaelekea katika msimu mpya wa ligi, hivyo ni vema mafunzo hayo ya vongozi wa klabu wakayafanyia kazi kwa mustakabali wa klabu zao.

Aidha, alisema chini ya uongozi wake umejikita zaidi katika kukuza na kuzalisha soka la vijana kuanzia madaraja ya chini ili kupata wachezaji wazuri wa timu za taifa kwa hapo baadaye.

Hata hivyo, viongozi hao wameahidi kutoa kipaumbe kwa kuzifundisha timu za vijana kwa misingi ya nidhamu na sheria za soka ili kupata wachezaji wazuri na wenye nidhamu.

Kwa upande wake mratibu wa michezo katika jimbo hilo la Kwahani, Alawi Haidar Foum alisema lengo la mafunzo hayo ni kukumbushana uongozi katika masuala ya mpira licha ya changamoto zilizopo katika kuzisimamia timu zao.

## Shimmuta kutimua vumbi Novemba

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma, Taasisi na Kampuni Binafsi (Shimmuta), yanatarajiwa kufanyika Novemba 18, mwaka huu mkoani Mwanza, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa mashindano hayo, Khamis Mkanacha alisema, yatashirikisha washiriki 1000.

"Mashindano ya mwaka huu yatakuwa ya aina yake kutokana na maazimio tuliyojiwekea,"alisema Khamis.

Hata hivyo, aliongeza yatatumia bajeti ya Sh. milioni 46, kutokana na kwamba mwaka huu washiriki wataongezeka.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kuhakikisha kila mfanyakazi anafanya mazoezi sehemu yake ya kazi ili kujenga afya ya mwili na kwamba kila taasisi itatoa washiriki 35 hadi 40 badala ya 24 wa mwaka jana.

# SOKA MWANZO MWISHO KUPITIA DSTV YAZINDULIWA

**Na Mwandishi Wetu**

SOKA Mwanzo Mwisho! Hiyo ndiyo kaulimbiu mpya ya msimu mpya wa soka kutoka DStv baada ya kuzinduliwa jana kuelekea Ligi Kuu mbalimbali kutarajiwa kuanza kunguruma mwishoni mwa wiki hii.

**Kabla ya uzinduzi huo, joto la msimu mpya lilizidi kupamba moto kutokana na maelfu ya mashabiki wa soka kote nchini kusubiri kwa hamu tangazo kutoka DStv ili kujua kama bado wataendelea kupata uhondo wa ligi maarufu duniani kupitia DStv.**

Hata hivyo, joto hilo lilishushwa ghafla jana baada ya Kampuni ya MultiChoice kutangaza rasmi kuwa kama ilivyo ada king'amuzi cha DStv kitarusha mubashara mitanange ya ligi maarufu duniani ikiwamo Ligi Kuu ya England (EPL), Italia (Serie A ), Hispania (La Liga), Ligi ya Mabingwa Ulaya (Uefa Champions League) pamoja na makombe mengine maarufu duniani.

Pazia la msimu huu mpya wa soka kwa England litafunguliwa Jumapili ya Agosti 2, kwa mtanange wa Ngao ya Jamii kati ya Liverpool na kigogo wa Ligi ya Kuu, Manchester City mchezo ambao utaonyeshwa mubashara kupitia DStv.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa msimu mpya wa soka iliyofanyika katika Hotel ya New Africa jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Masoko wa kampuni hiyo, Ronald Shelukindo, alisema msimu huu wa soka, DStv inawahakikishia wateja wake wote kuendelea kuliona soka katika muonekano bora zaidi huku wakiweza kufuatilia ligi ya England itakayorushwa kwa lugha ya Kiswahili.

"Kampeni yetu ya sasa tunasema 'Mwaaa... Mwiii' ndani ya DStv, tukiwa na maana 'Soka Mwanzo Mwisho' na tunamaanisha kwani kwa wateja wetu wa DStv, burudani ya soka haitawatindikia kamwe! Ni wapi unaweza kuona mechi zote 380 za ligi ya Uingereza, mechi 380, za Ligi Kuu ya Hispania, mechi 380 za Ligi Kuu ya Italia bila kusahau mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya na nyingine nyingi? Bila shaka ni DStv pekee.. ndiyo sababu tunasema kwetu DStv ni Soka Mwanzo Mwisho!

"Katika kuhakikisha kuwa burudani hiyo haimpiti mteja wa DStv, kwa kupitia 'app ya DStv Now' wateja wataweza pia kuangalia popote walipo wakati wowote kwa kutumia vifaa kama simu, tablet na laptop," alisema Shelukindo.

Alisema mteja anayetumia DStv Now anaweza kuunganisha vifaa vinne tofauti kwa kutumia akaunti moja bila malipo ya ziada.

Uzinduzi huo pia ulihudhuriwa na wadau wa soka nchini wakiwamo wasanii mbalimbali, wachezaji wastaafu na watangazaji wanaotangaza Ligi Kuu ya England kwa Kiswahili ambao ni Salama Jabir, Edo Kumwembe, Abuubakar Lyongo na Oscar Oscar, wengine wanaotangaza ambao walikuwa na dharura ni Ibrahim Masoud (Maestro) na Maulid Kitenge.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wadau hao wa soka wamesema kitendo cha DStv kuonyesha ligi hizo kubwa mubashara ni fursa kubwa siyo kwa mashabiki tu wa soka bali pia hata kwa wanasoka wenyewe kwani ni ulingo muhimu wa kujifunza.

Sambamba na uzinduzi wa kampeni hiyo, DStv pia imetangaza ofa maalum kwa wateja wapya wanaojiunga kuanzia Agosti Mosi hadi Septemba 30, mwaka huu kuwa watajiunga na DStv kwa Sh. 99,000 / -na kupata kifurushi cha Family cha miezi miwili




Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso (wa pili kulia), akifurahi jambo na Mkuu wa Masoko, Ronald Shelukindo pamoja na watangazaji watakaotangaza michuano ya Ligi Kuu ya England kwa Kiswahili – Salama Jabir (kushoto) na Aboubakar Lyongo (kulia) wakati wa uzinduzi wa kampeni ya msimu wa soka ya DStv ijulikanayo kama 'Soka Mwaaa-Mwiii... ndani ya DStv'. DStv imetangaza kuwa itarusha mubashara ligi maarufu duniani ikiwamo ya England, Hispania, Italia pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *JWTZ 105 wapania michuano Majeshi*

**Na Mary Geofrey**

MICHUANO ya Majeshi katika nchi sita za Afrika, inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Agosti 12 hadi 24, mwaka huu, jijini Nairobi nchini Kenya huku Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), likitarajia kupeleka viongozi na wachezaji 105.

Katika kuhakikisha Tanzania inashiriki kikamilifu michuano hiyo, Benki ya NMB imetoa udhamini wa vifaa vya michezo ikiwamo jezi na mipira vyenye thamani ya Sh. milioni 15.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi, Brigedia Jenerali, David Mallugu, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhiwa vifaa hivyo jana jijini Dar es Salaam, alisema JWTZ inapeleka washiriki wa michezo mitano.

Alitaja michezo watakayoshiriki kuwa ni mpira wa miguu, mpira wa pete, mpira wa kikapu, riadha na mbio za magongo.

"Tunaishukuru NMB kwa kuendelea kutudhamini katika michuano hii muhimu kwetu sisi, tunaahidi tutarudi na ushindi wa jumla, la sivyo tutarudi na vikombe vingi zaidi kwa sababu tumejiandaa kikamilifu kwa kupeleka timu za michezo mingi tofauti na nchi nyingine," Brigedia Jenerali Mallungu alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo Huduma Binafsi wa NMB, Omary Mtiga, alisema ni mara ya nne benki hiyo inaendelea kufadhili michuano hiyo ya majeshi.

Alisema wanawatakia kila la heri katika michuano hiyo huku wakiamini kuwa timu hiyo itarudi na ushindi hivyo kuendelea kupeperusha bendera ya Tanzania kimataifa.

# Michezo

Jumamosi Agosti 3, 2019


Nipashe




Mbappe amshauri Neymar kubaki PSG

UKURASA 30

MINOTI...




Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 100 na Mkurugenzi Mkuu wa SportPesa, Pavel Slavkov, kufuatia klabu hiyo kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara. Kushoto ni Mkurugenzi wa Utawala na Utekelezaji SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas. **PICHA: SPORTPESA NEWS**

## Simba wajazwa tena mamilioni

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA kilele cha SportPesa Simba Wiki, klabu hiyo imezidi kushukiwa na neema baada ya jana kukabidhiwa Sh. milioni 150,000 kutoka kwa mdhamini wao mkuu Kampuni ya SportPesa, kwa kufanikiwa kuingia robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu uliopita.

Akizungumza jana wakati wachezaji wa timu hiyo walipofanya ziara ofisini kwake, Mkurugenzi wa Utawala Na Utekelezaji SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema ametoa fedha hizo kwa Simba kutokana na juhudi kubwa wachezaji waliyoifanya.

Alisema Sh. milioni 50 ni kutokana na timu hiyo kufanikiwa kuingia hatua ya robo fainali kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa na Sh. milioni 100 ni kwa ajili ya kutwaa Kombe la Ligi Kuu Bara msimu uliopita, na kueleza wao kama wadhamini wameridhishwa na kiwango walichokionyesha.

"Nawapongeza Simba kutokana na juhudi waliyoifanya katika mashindano yote waliyoyafanya ikiwa ni pamoja na kujaza uwanja wakati walipokuwa wanacheza,"alisema Tarimba.

Aidha, aliwataka wachezaji wa Simba kuongeza juhudi zaidi msimu ujao ili wazidi kutetea ubingwa huo kutokana na dalili kuonyesha msimu huu utakuwa na ushindani mkubwa, kufuatia maandalizi mazuri yaliyofanywa na timu zote.

# Yanga yainogesha Siku ya Mwananchi

**Na Shufaa Lyimo**

### ●●● Historia mpya kuandikwa ikiivaa Kariobangi Sharks kesho Uwanja wa Taifa na uzi mpya, warejea Dar huku...



Kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera.

IKIWA imebaki siku moja kuelekea kilele cha Siku ya Mwananchi, Klabu ya Yanga imezidi kunogesha kilele hicho baada ya jana kuzindua uzi mpya uliotengenezwa na Kampuni ya GSM ambao utaanza kutumika rasmi kesho na kuendelea nao msimu mpya wa michuano ya kimataifa na Ligi Kuu Bara unaotarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu.

**Akizungumza na waandishi wa habari jana katika uzinduzi huo, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mshindo Msolla, alishukuru kwa kufanikiwa kuzindua jezi hizo licha ya kukalia kiti hicho kwa muda mfupi tangu achaguliwe kuiongoza Yanga.**

Alisema jezi hizo zimetengenezwa kwa ubora wa hali ya juu tofauti na kipindi cha nyuma ambapo baadhi ya watu walinufaika kwa kuziuza visivyo halali na kwamba kwa sasa klabu itanufaika na kuwataka wanachama wa timu hiyo kuacha kununua jezi ambazo hazina lebo ya Yanga.

"Wakati nilipokuwa nafanya kampeni ili kuchaguliwa kuitumikia klabu hii mashabiki wengi waliniambia hawawezi kununua jezi za Yanga kwa sababu klabu yao hainufaiki na kitu chochote kile sasa tumeleta jezi halali," alisema Msolla.

Alisema jezi hizo zimeanza kuuzwa jana mara tu baada ya kuzinduliwa na kuishukuru Kampuni ya GSM kuwaletea jezi zenye ubora wa hali ya juu ambazo hazijawahi kutumika hapa nchini, zitakazokuwa zikipatikana katika maduka ya kisasa pamoja na makao makuu ya klabu hiyo, Jangwani Jijini Dar es Salaam. Alisema maduka yatakayotumika kuuza jezi hizo yatakuwa Pugu, Msasani na kudai fedha zote zitakazopatikana zitakuwa faida ya klabu.

"Jezi ya njano itakuwa inavaliwa ugenini (away) na jezi ya kijani itakuwa ya nyumbani, naamini tumefanya mapinduzi ambayo hayana mpinzani ,sasa hivi jezi za vichochoroni haziruhusiwi tena,"alisema mwenyekiti huyo.

Kuhusu maendeleo ya timu alisema kikosi kiliwasili jana jioni kikitokea mkoani Morogoro kilipokuwa kimeweka kambi kwa ajili ya msimu ujao Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa pamoja na mchezo wao wa kuhitimisha kilele cha Siku ya Mwananchi watakapokutana na timu ya Kariobangi Sharks ya Kenya mchezo ambao utachezwa Uwanja wa Taifa kesho, Jumapili.

"Tunategemea kuipokea timu yetu leo (jana) jioni ikitokea Morogoro tayari kwa ajili ya mchezo wetu wa kirafiki dhidi ya Kariobangi Sharks kwenye kilele cha Siku yetu ya Mwananchi ambapo kila shabiki na mwanachama atafanikiwa kuona wachezaji wapya tuliowasajili,"alisema kiongozi huyo.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Kampuni ya GSM, Said Hers, alisema wameingia mkataba wa mwaka moja na Yanga kuwatengenezea bidhaa zao na kudai zoezi hilo litakuwa endelevu. Mkurugenzi huyo alisema jezi hizo zimetengenezwa kwa ufanisi mkubwa na kwamba watasajili mawakala mbalimbali ambao watatumika kuuza jezi hizo zikiwa na lebo ya GSM .

"Hizi jezi tumezitengeneza kwa ubunifu wa hali ya juu, haziwezi kuchakachuliwa kama zilivyokuwa zinafanywa kwenye zile zilizokuwa zinatumika msimu uliopita, tunakwenda kuweka historia siku hiyo ikifika,"alisema Said.



9 770856 541002